# UCHANGANUZI WA MATINI TEULE YA NYIMBO ZA FOUSTINE MUNISHI: MTAZAMO WA NADHARIA YA UPOLE

NA

OWINO MARTHA A.

C50/77599/09

TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KITIVO CHA SANAA IDARA YA ISIMU NA LUGHA KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2011

University of NAIROBI Library

0496790 7

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa na mtu yeyote kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili au uzamifu katika Chuo Kikuu cha Nairobi au chuo kingine kikuu chochote au taasisi yoyote.

______________

**Owino Martha A.** **Tarehe** — 27/10/2011

**TASNIFU HII IMETOLEWA KUTAHINIWA KWA IDHINI YETU KAMA WASIMAMIZI WA KAZI HII KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**MSIMAMIZI: PROF. JOHN HABWE**

**SAHIHI:** ______________

**TAREHE** 27/10/2011

**MSIMAMIZI: Bi. HANNAH MWALIWA**

**SAHIHI:** ______________

**TAREHE:** 27th October, 2011

# TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia mamangu mpendwa Jane Owino pamoja na marehemu babangu Charles Owino kwa kunilea na kunipeleka shule huku wakinitia moyo kuwa ingawa jitihada haiondoi kudra, lakini ni muhimu kuwa na bidii maishani.

Pia naitabarukia mume wangu mpenzi aliye pia rafiki wangu wa karibu Joshua Ogal pamoja na wanangu Emmanuel Charles na Victor Angel kwa kuvumilia mateso yaliyotokana na usomi wangu. Safari hii ilionekana ndefu lakini mlinitia moyo na kuniombea kila mara, mlivumilia kuwa na mama msomi na mkawa nami hadi mwisho. Nawatakieni baraka za Mwenyezi Mungu nanyi muweze kupata ufanisi kwa yote mtendayo.

## SHUKRANI

Natoa shukrani kwa wale wote waliochangia ufanisi wa kazi hii kwa njia moja au nyingine.

Kwanza kabisa, shukrani ni kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya, uhai, uvumilivu, maarifa na hata kunipa rasilimali niliyotumia katika kutimiza ndoto yangu ya kupata shahada ya uzamili. Neema za Mungu zimenifaa kuliabiri jahazi hili la usomo hadi tamati. Kwa kweli, neema hiyo imenifaa namna petroli inavyofaa gari ili liweze kusonga.

Nawashukuru wahadhiri wote wa idara ya isimu na lugha kwa mchango wao kupitia ushauri walionipa na kwa kunifunza somo la Kiswahili. Mlinionyesha moyo wa wema na hekima, na kila mara mlihakikisha tumepata elimu ya kutosha, na mlituhimiza tuwe na jitihada katika kudurusu vitabu kadha ili tupanue uelewa wetu katika somo la Kiswahili.

Ni dhahiri kwamba nyote muliotufunza mlitufaa pakubwa. Ninawashukuru nyote mliotusaidia katika masomo yetu ambao ni pamoja na: Prof. John Habwe, Prof. Abdulaziz, Dkt. Buregeya, Dkt. Kineene wa Mutiso, Dkt. Mukhwana, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Mwenda Mbatia, Dkt. Tom Olali na Bwana Basilo G. Mungania.

Shukrani zangu za dhati nazitoa kwa wasimamizi wangu Profesa John Habwe na Bi. Hannah Mwaliwa. Msaada wenu wa kuniongoza na kunirekebisha kila uchao ulinifaa sana katika kukamilisha tasnifu hii. Ushauri wenu wa kitaaluma ulinisaidia kufika mwisho wa safari hii. Maneno hayatoshi kuwashukuru bali tu naomba Mwenyezi Mungu awabariki na kuwapa neema ya kuwasaidia wengine watakaohitaji msaada wenu.

Kamwe siwezi kuwasahau wenzangu ambao tumeabiri jahazi moja la kutafuta elimu ya juu na kuhakikisha tumefika mwisho wa safari licha ya mawimbi makali baharini. Tumepitia mengi ambayo yalikuwa yakututia moyo na wakati mwingine tukivunjika moyo hadi karibu kufikia kiwango cha kukata tamaa lakini tulihimizana na kusaidiana kwa hali na mali ili kuhakikisha kuwa hakuna mmoja wetu angelemewa na safari hii. Hongera kwenu nyote kwa juhudi zenu hadi tamati. Tuliokuwa nao katika darasa la Kiswahili ni pamoja na: Julius Shitemi, Chrispinus Wanyonyi, Patrick Okombo, Mirikau Suleiman, Paul Kamotho, Hannington Gitonga, Peter Thamu, John Paul Warambo na Jacob Maobe.

Vilevile nawashukuru wale wengine ambao tulikuwa nao katika idara ya isimu na lugha kwa msaada wao haswa wa vitabu na mijadala ambayo ilinifaa sana katika kozi hii. Nawashukuru ndugu zangu walionitia moyo wa kuendelea, kwani walinihimiza kuwa mtaka cha mvunguni sharti ainame. Kweli ari yao ilikuwa ni kuona dada yao wa pekee akifanikiwa kupata shahada ya uzamili. Dua langu ni Mungu awabariki na kuwatunukia neema yake ili waishi maisha marefu.

Pia nashukuru tume ya kuajiri walimu (TSC) kwa kuniruhusu kuendelea na masomo haya na hata kunipa likizo ili niweze kusoma chuoni mfululizo.

Nakishukuru Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kuniruhusu kujiunga nacho kwa masomo ya shahada ya uzamili. Mipango yake kabambe imeniwezesha kukamilisha masomo yangu kwa muda uliowekwa.

Shukrani tele kwa wale wote walionifaa katika kufanikisha kazi hii. Ingawa sikuwataja , wema wenu haujasahaulika. Moyo wangu umejaa shukrani na ombi langu ni kuwa Mwenyezi Mungu awabariki nyote nanyi mpate kibali na wengine mnapohitaji msaada wowote ule.

**IKISIRI**

Utafiti huu ulishughulikia uchanganuzi wa matini teule ya nyimbo za Foustine Munishi-mtazamo wa nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) hasa kipengele cha mikakati ya kuokoa uso.

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kubainisha suala la upole katika matini teule ya nyimbo mbili za Foustine Munishi. Foustine Munishi alizingatia upole katika kutunga nyimbo zake tulizoteua.

Katika sura ya kwanza, tulieleza kwa ufupi kuhusu usuli wa mada ya utafiti. Tulieleza tatizo la utafiti na kuorodhesha madhumuni na nadharia tete za utafiti huu. Katika sura hii pia tulishughulikia sababu za kuchagua mada, upeo wa utafiti, msingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na njia za utafiti. Tulitumia mbinu ya maktabani katika kukusanya data tuliyohitaji na kuichanganua. Tulithibitisha kuwa kuna mikakati mbalimbali ya kuokoa uso chanya na uso hasi kwenye matini teule ya nyimbo mbili za Munishi.

Katika sura ya pili tulishughulikia nyimbo; aina na majukumu kwa jumla na mtindo. Katika sura ya tatu tulibainisha suala la upole katika nyimbo za dini kwa ujumla. Pia tulieleza suala la upole katika matini teule ya wimbo wa Munishi: wimbo wa *Maji yana mdudu*. Katika sura ya nne tulibainisha suala la upole katika matini teule ya wimbo wa Munishi: wimbo wa *Malebo*.

Hitimisho na mapendekezo yametolewa katika sura ya tano.

# YALIYOMO

IKIRARI ..... ii
TABARUKU ..... iii
SHUKRANI ..... iv
IKISIRI ..... vii
YALIYOMO ..... viii
**SURA YA KWANZA ..... 1**
1.0 MUHTASARI ..... 1
1.1 UTANGULIZI ..... 1
1.2 USULI WA MADA YA UTAFITI ..... 2
1.3 TATIZO LA UTAFITI ..... 3
1.4 MALENGO YA UTAFITI ..... 4
1.5 NADHARIA TETE ..... 4
1.6 SABABU ZA KUCHAGUA MADA ..... 4
1.7 UPEO NA MIPAKA ..... 5
1.8 MSINGI YA NADHARIA ..... 6
1.8.1 Uso hasi ..... 9
1.8.2 Uso chanya ..... 9
1.8.3 Mahitaji ya uso. ..... 10
1.8.4 Mikakati ya kuheshimu nyuso ..... 10
1.8.5 Upole chanya ..... 11
1.8.6 Upole hasi ..... 11
1.8.7 Mkakati wa rekodi ..... 12
1.8.8 Kuwa kwenye rekodi ..... 13
1.8.9 Kuwa nje ya rekodi ..... 13
1.9 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA ..... 15
1.10 MBINU ZA UTAFITI ..... 21
1.10.1 Eneo la Utafiti ..... 21
1.10.2 Sampuli ..... 21
1.10.3 Nyenzo za Utafiti ..... 22
1.11 UCHANGANUZI WA DATA ..... 22

1.12 UMUHIMU WA UTAFITI ........ 22
1.13 HITIMISHO ........ 23
**SURA YA PILI ........ 24**
**NYIMBO; AINA NA MAJUKUMU. ........ 24**
2.0 UTANGULIZI ........ 24
2.1 NYIMBO ........ 24
2.2 AINA ZA NYIMBO ........ 27
2.3 MAJUKUMU YA NYIMBO NA VIPENGELE VYA KIMUKTADHA ........ 28
2.3.1 Nyimbo za sherehe ya kuzaliwa ........ 29
2 3.2 Nyimbo za kumpa mtoto jina ........ 29
2.3.3. Bembelezi/ Bembe/ Bembezi ........ 29
2.3.4 Nyimbo za dini ........ 30
2.3.5. Nyimbo za nyiso/ tohara ........ 30
2.3.6 Nyimbo za watoto ........ 31
2.3.7 Nyimbo za harusi ........ 32
2.3.8 Nyimbo za mapenzi ........ 32
2.3.9 Nyimbo za kazi (Hodiya) ........ 33
2.3.10 Nyimbo za matanga/mbolezi ........ 34
2.3.11 Nyimbo za kishujaa ........ 34
2.3.12 Nyimbo za kizalendo ........ 35
2.3.13 Nyimbo za tambiko ........ 35
2.14 HITIMISHO ........ 36
**SURA YA TATU ........ 37**
**UCHANGANUZI WA MASUALA YA UPOLE KATIKA MATINI TEULE YA NYIMBO ZA MUNISHI: MTAZAMO WA NADHARIA YA UPOLE YA BROWN NA LEVINSON ........ 37**
3.0 UTANGULIZI ........ 37
3.1 SUALA LA UPOLE KWENYE NYIMBO ZA DINI KWA JUMLA ........ 37
3.2 UPOLE KWENYE MATINI TEULE YA NYIMBO ZA MUNISHI: WIMBO WA MAJI YANA MDUDU ........ 38
3.3 UPOLE CHANYA ........ 39

3.4 UPOLE HASI .......... 44
3.5 KUWA NJE YA REKODI .......... 45
3.6 KUWA KWENYE REKODI .......... 45
3.7 HITIMISHO .......... 46
**SURA YA NNE .......... 47**
4.0 UPOLE KWENYE MATINI TEULE YA NYIMBO ZA MUNISHI: WIMBO WA MALEBO .......... 47
4.1UTANGULIZI .......... 47
4.2 UPOLE CHANYA .......... 50
4.3 UPOLE HASI .......... 51
4.4 KUWA NJE YA REKODI .......... 52
4.5 KUWA KWENYE REKODI .......... 53
4.6 HITIMISHO .......... 54
**SURA YA TANO .......... 55**
**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .......... 55**
5.0 UTANGULIZI .......... 55
5.1 HITIMISHO .......... 55
5.2 CHANGAMOTO TULIZOKUMBANA NAZO KATIKA UTAFITI WETU .......... 57
5.3 MAPENDEKEZO .......... 59
MAREJELEO .......... 60
VIAMBATISHO .......... 63

## SURA YA KWANZA

### 1.0 MUHTASARI

Sura hii inashughulikia maswala muhimu yanayohitajika katika utafiti huu. Tumeelezea usuli wa mada ya utafiti kwa kuangazia suala la upole katika nyimbo teule za mwimbaji Foustin Munishi. Pia tumeshughulikia tatizo la utafiti na malengo ya utafiti huu. Kisha tumeelezea nadharia tete na sababu za kuchagua mada. Kisha tumeshughulikia upeo na mipaka ya utafiti, msingi wa nadharia na yaliyoandikwa kuhusu mada. Hatimaye tumeangazia mbinu za utafiti na umuhimu wa utafiti.

### 1.1 UTANGULIZI

*New International Webster Comprehensive Dictionary* (2001), inafafanua wimbo kama "shairi fupi inayonuiwa kuimbwa au kutoimbwa." Fasili hii ni muhimu sana katika uyafiti huu kwa sababu ina kipengele cha uimbaji.

Beja (2000:1) anasema nyimbo ni mashairi yaliyotungwa kuimbwa katika sherehe rasmi au zisizo rasmi na huimbwa na watu au waimbaji binafsi au na makundi ya watu.

Timammy (2002:1) anasema kuwa 'wimbo ni tamko lenye mahadhi lililo na beti moja au zaidi yenye maana kamilifu kimuktadha. Maana hii inawiana na mada yetu ya uchunguzi. Katika mahusiko yetu tutachagua nyimbo zenye umaarufu kimaudhui, na yenye upole katika uwasilishi.

Kwa mujibu wa *Oxford Online Dictionary*, wimbo maarufu ni ule ambao usemi wake umekita katika tamaduni pendwa ya kisasa na katika vyombo vya habari. Wimbo ni njia muhimu ambayo jamii kupitia kwa wasanii wa nyimbo huhifadhi vipengele vya mabadiliko ya kijamii ili wapate kufahamu changamoto wanayopitia. Aidha kufuatia kuvumbuliwa kwa jamii za kiafrika kutoka kwa tamaduni zao za kikabila, miktadha nyingi ya uigizaji imepotezwa, na ni kutokana na sababu hii ndipo nyimbo maarufu huwa muhimu kwa kutekeleza jukumu hili. Nyimbo za

Munishi ni maarufu sana kutokana na ujumbe wake ambao anapitisha kwa uzito lakini katika hali ya upole.

## 1.2 USULI WA MADA YA UTAFITI

Foustin Munishi ni mwinjilisti na mwimbaji wa nyimbo za injili. Alizaliwa Arusha, nchini Tanzania ambapo miaka 44 iliyopita alikuwa akifanya kazi ya kupaka rangi. Alibadili kazi mwaka wa 1980 alipookoka na kuanza kuimba nyimbo kama 'Niko chini ya mwamba," wimbo uliotia fora sana nchini Kenya mwaka wa 1990.

Wimbo huo ndio alianza nao kazi ya uimbaji na kwa hakika aliweza kufanya biashara yenye faida tele kutokana na kuuza kanda hiyo. Katika utafiti huu, tumeteua nyimbo mbili, "maji yana mdudu" na "malebo" ambazo zimo katika kanda zake tofauti za muziki, na nyimbo hizo zimeimbwa kwa lugha ya Kiswahili.

Katika miaka ambayo Munishi anaandika na kuimba nyimbo hizi kulikuwa mambo mengi yaliyokuwa yakitendeka katika mazingira ya Kenya na Afrika kwa Jumla. Ni wakati janga la ukimwi lilikuwa limeandama nchi ya Kenya. Aidha kwa sababu ya ukosefu wa habari tosha janga hili lilichukuliwa kwa njia tofauti na jamii mbalimbali. Kuna baadhi ya watu katika jamii ambao hawakuamini ukimwi ni ugonjwa. Badala yake walichukulia ugonjwa huu kama jambo la urogi, laana, tukio la visa vya miiko na bahati mbaya na nuksi. Hivyo walioangukiwa na janga hili hawakujitokeza wazi kwa sababu ya unyanyapaa uliohusishwa na Janga hili. Pamoja na kwamba Janga hili halikuzungumziwa waziwazi, ulizidi kuenea. Washika dau ambao walipaswa kuwajibikia janga hili hawakulishughulika. Kutokana na kutowajibika, waimbaji na wasanii

walitunga na kuimba nyimbo zilizobeba ujumbe wa janga hili. Hata hivyo, kutokana na uzito wa maudhui haya, iliwabidi waimbaji watumie mikakati ya aina yake ilimradi nyimbo hupokelewe kwa upole. Munishi Foustin ndiye miongoni mwa waimbaji hawa walioimba nyimbo zenye ujumbe huu. Ndiposa akaimba wimbo "maji yana mdudu ambao umesheheni mkakati wa upole kwa hali ya juu sana kama tutakavyoona baadaye katika sura ya uchanganuzi wa data.

Kutokana na hali hii vigeuzi vya maadili vya jamii vilikuwa vimeporomoka vikiwemo urafiki baina ya wanajamii, uadilifu wa kidini, upujufu wa mienendo na taratibu kubalifu za jamii. Kutokana na msingi huu ndipo Munishi anatunga na kuimba nyimbo tulizoteua. Tumevutiwa kufanya utafiti huu kwa njia anayotumia tafsida katika uwasilishi wake. Kwa jumla, nyimbo hizi mbili zimekuwa zenye kuvutia kwa utajiri wao wa kimawazo.

### 1.3 TATIZO LA UTAFITI

Dini imechukua nafasi kubwa katika jamii tangu zamani. Hata hivyo masuala ya dini na imani za watu huwa na mahusiano tata hasa katika upande wa matumizi ya lugha kama inavyodhihirika kupitia kwa nyimbo. Kila jamii huwa na imani fulani zinazoiendesha katika shughuli za kila siku maishani mwao. Nyimbo katika dini huchukua nafasi kubwa sana. Nyimbo za dini huimbwa kwa mkakati fulani ili kuokoa nyuso za wanaohusika. Wasomi na watafiti mbalimbali wa fasihi simulizi wameshughulikia baadhi ya tanzu za fasihi simulizi zinazohusiana na shughuli za harusi, jando na matanga. Hata hivyo hapajakuwa na mtafiti ambaye ameshughulikia suala la upole kwenye nyimbo hata ukiachilia mbali nyimbo za dini hasa kwa kutumia nadharia ya upole ya Penolpe Brown na Levinson ya uso. Hivyo bado kuna mwanya ulioachwa kwa ukosefu wa

habari hizi. Kwa hivyo tatizo la utafiti wetu ni kubainisha suala la upole katika matini teule ya nyimbo za Foustine Munishi.

## 1.4 MALENGO YA UTAFITI

Malengo ya utafiti huu ni kama yafuatayo:

1. Kuchanganua mikakati ya upole chanya katika nyimbo mbili teule za Munishi.
2. Kuchanganua mikakati ya upole hasi, kwenye rekodi na nje ya rekodi katika nyimbo mbili teule za Munishi.

## 1.5 NADHARIA TETE

Utafiti huu utaongozwa na nadharia tete zifuatazo:

1. Kuna mikakati ya upole chanya katika nyimbo mbili teule za Munishi.
2. Kuna mikakati ya upole hasi, kwenye rekodi na nje ya rekodi katika nyimbo mbili teule za Munishi.

## 1.6 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Fasihi ni fani hai na ambayo inaendelea kutekeleza majukumu muhimu katika jamii. Nyimbo kama asemavyo Wamitila (2003) zinatekeleza majukumu muhimu katika maisha ya kila siku. Maadili yalikuzwa na hata sasa yanakuzwa kwa kupitia nyimbo za dini. Licha ya ukiukaji wa maadili na kuacha mila miongoni mwa vizazi vya leo, nyimbo huchangia katika kujaribu kuwaelimisha wanajamii umuhimu wa kuwa na maadili mema. Nyimbo hutumiwa pakubwa kupitisha ujumbe wa kidini, na ni sehemu muhimu sana katika ibada ya kikristo. Nyimbo hizi hutumia kushawishi, kuelekeza, kufundisha na hata kuhubiri ili. Ili kufanya nyimbo hizi kutumia

ufundi wa juu wa lugha, msanii hulazimika kuteua maneno kwa makini. Kwa sababu hiyo nyimbo katika muktadha wa kidini hujitokeza kama diskosi iliyokamilifu. Kwa kurejelea majukumu yanayotekelezwa na nyimbo katika jamii, ni dhahiri kwamba kwa kubainisha majukumu haya, tutakuwa tumeelezea nafasi ya nyimbo za Munishi katika jamii kwa kutumia nadharia ya upole, tutajaribu kutafuta namna mwimbaji anavyookoa nyuso za wasikilizaji kwa kutumia lugha. Anaposema:

"Uchimbe kisima wewe mwenyewe unywe maji yako peke yako na usiyashiriki nao wengine ni hatari kubwa eeh!

Hapo anawasilisha ujumbe kwa kutumia tamathali za lugha, huku akihimiza wanajamii kuwa waaminifu katika ndoa zao. Utafiti huu unanuiwa kuangazia nyimbo za Munishi na kuweka wazi umilisi wa kimawasiliano alio nao katika kuwasilisha ujumbe wa kijamii katika nyimbo za kikristo. Pamoja na hayo tulichagua mada hii kwa kuvutiwa na matumizi kitamathali katika nyimbo hizi. Zaidi tulipendezwa na upole unavyojidhihirisha katika nyimbo hizi.

## 1.7 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu umekita katika nyimbo za kidini, hasa nyimbo mbili teule zilizoimbwa na Foustin Munishi. Tumechagua nyimbo mbili za Munishi kwa sababu nyimbo zote za dini huwa na ujumbe na malengo yanayofanana na Munishi ni baadhi ya waimbaji wa zamani mashuhuri wa nyimbo za dini.

## 1.8 MSINGI YA NADHARIA

Nadharia tuliyoitumia katika utafiti wetu ni ya upole ya Penelope Brown na Stephen Levinson (1987). Kinadharia utafiti huu unahusiana na uwanja na pragmatiki ambao huhusika na unenaji na wala sio sentensi. Nadharia ya upole ilitusaidia kuchanganua maneno yanayotumiwa kwenye nyimbo kama mkakati wa upole katika kuwasilisha ujumbe.


Brown na Levinson walikuwa wanaanthropolojia kule uingereza. Nadharia hii iliandikwa baada ya Erving Goffman (1963) kuchapisha makala juu ya 'Kazi za uso.' Ndiye aliyekuwa mwasisi wa dhana ya uso ambayo ilichochea kuwepo kwa nadharia ya upole. Kulingana naye Goffman, dhana hii ya 'uso' ilitokea uchina ambapo aliikopa na ambayo ilitumika kuashiria hali ambapo mzungumzaji au msikilizaji angetaka hali yake katika mawasiliano yadumishwe. Anasema kila mtu ana uso wake unaobainisha yeye kama yeye. Pia binadamu ana uso wa hadhira na uso wa hadhira si wake. Anafafanua 'uso' kama kitu muhimu cha kijamii ambacho mtu anadai kwa namna ambayo wengine wanachukulia amekipata wakati wa mtagusano fulani katika jamii. Goffman (1967:5) anasema; 'uso si kitu cha kibinafsi kilichomo ndani au nje ya mwili wa mtu, bali ni ishara inayopatikana katika mtiririko wa matukio inayothibitishwa na maamuzi ya watu wengine na nguvu inayojibainisha katika hali ya mtagusano katika jamii. Kwa hivyo, 'uso' ambayo ni ishara bayana katika jamii ni sharti kuthaminiwa. Nadharia ya upole (politeness Theory) ni nadharia ya kuokoa uso (Face saving Theory) kutokana na matendo ya kutishia uso (Face Threatening Acts ) katika mitagusano ya kijamii. Brown na Levinson wanasema dhana ya uso ni muhimu katika maingiliano ya binadamu. Pia walitambua kuwa kuna vitisho mbalimbali vya uso. Brown na Levinson wanasema dhana ya uso ni muhimu katika maingiliano ya binadamu. Pia walitambua kuwa kuna vitisho mbalimbali vya uso katika maingiliano (Face

Threatening Acts) kulingana nao, binadamu yafaa awe na uso kwa sababu katika lugha binadamu anataka kuthaminiwa, hataki kupoteza uso wake, anataka kuuhifadhi.

Vitisho vya uso ni vya aina zifuatazo:

a) Ukosefu upole hasi (Negative impoliteness)

b) Ukosefu upole chanya (positive impoliteness)




Kutokana na vitisho hivyo, Brown na Levinson waliona ni lazima pawe na mbinu na mikakati ya kuokoa nyuso hizi ili kudumisha maingiliano. Hivyo, walipendekeza mbinu tatu;

1. Kuwa nje ya rekodi na kuwa ndani ya rekodi. Kuwa nje ya rekodi ni kusema vitu, mambo kwa mafumbo mbalimbali lakini sio waziwazi yaani, kujaribu kuokoa uso kwa kutumia lugha, kuwa ndani ya rekodi ni kusema mambo waziwazi pasipo na kufinyanga lugha.

2. Mikakati ya upole hasi

Katika mkakati huu mzungumzaji huenda akaingilia msikilizaji wake na kuzua hali ya kumkera. Huwa kuna uwezekano wa kudhuru hisia za hadhira inayozungumziwa.

3. Mikakati upole chanya

Ni mkakati wa kumtambua mtu kumsifu, kumshirikisha au kumshukuru mtu.

Mikakati hii inatofautiana katika tamaduni mbalimbali.

Nadharia hii pia imechota malighafi yake kutoka kwa kazi yake Leech (1986) inayohusu kanuni za upole (politeness maxims). Kanuni hizi nazo zimetokana na kuimarishwa kwa misimamo ya ushirikiano yake Grice (Co-operation principle 1975). Kipengee cha uso chake Goffman ndio msingi wa nadharia ya upole. Kipengee hiki kinaonyesha kuwa huwa tunabadilisha lugha kutokana na msikilizaji na kuegemea mikakati ya upole kwa kuzingatia hadhira. Kulingana na Brown na Levinson huwa tunawasilisha ujumbe kila siku maishani ili kukinga au kuokoa uso na kufanikiwa katika mambo mengine. Wanaelezea 'uso' kuwa ni jinsi kila mtu anavyojibainisha mbele ya jamii na anavyodai kutoka kwa jamii katika mitagusano ya kijamii.

Hali ya kuwepo kwa tishio la uso wa mtu hujulikana kama Tendo la kutishia uso (Face Threatening Act). Tendo hili linahitaji kupunguza makali katika uneni au uneni wa upole kurekebisha au mazungumzo yatakosa kuafikiwa. Matamshi makali wakati mwingine husababisha tendo la kutishia uso, hivyo ni muhimu kwa mzungumzaji kuwa na ufahamu wa uchaguzi wa maneno katika uneni, na kutumia maneno kwa kufikiri kirazini huku akijali anayezungumzia. Mikakati ya upole hutumiwa ili kuelekeza ujumbe unaonuia kuokoa uso wa msikilizaji wakati Tendo la kutishia uso haliepukiki au vinahitajika (ufafanuzi wake Mill,: 2003: 12), kimsingi mzungumzaji huepuka kumkera anayemsikiliza.

Wanadamu wote wana uso wa aina mbili.

a) uso hasi

b) uso chanya.

### 1.8.1 Uso hasi

Kila mwanadamu hudai haki na uhuru katika jamii. Mwanadamu yeyote yule huwa hataki kuingiliwa, kuombwa au kukosa tendo la uhuru la mshiriki katika mazungumzo. Uso hasi unaweza kupotezwa iwapo mtu atajiingiza katika mambo ya mtu mwingine bila hiari yake, kumwomba mtu kitu chake ilhali hataki kuombwa au kujikaribisha kwa mtu ambaye hajisikii kukukaribisha.

Uso hasi hutishwa wakati mtu hakwepi au hatarajii kukwepa tendo la uhuru la mshiriki katika mazungumzo. Tendo hilo huenda likamdhuru mzungumzaji au hata msikilizaji na kumfanya mmoja wao kunyenyekea chini ya mwingine. Uhuru wa uchaguzi na kutenda huzuiwa wakati uso hasi umetishwa. Uso hasi ni uhitaji wa kutaka kusalia uhuru na ndio mzungumzaji atakuwa mwepesi wa kuwa na njia ya kumhusisha msikilizaji.

### 1.8.2 Uso chanya

Uso chanya hudhuriwa pale mzungumzaji au msikilizaji hajali hali ya yule wanayeingiliana naye. Kila mwanadamu angependa kusifiwa, kutobaguliwa au kushirikishwa katika shughuli za kijamii, hivyo mtu anapokosa kusifiwa au anapobaguliwa au kutoshirikishwa katika shughuli za jamii, huenda uso chanya ukadhuriwa.

### 1.8.3 Mahitaji ya uso.

Yule (1996:61) anarejelea dhana ya uso kama 'mahitaji ya uso' na kusema kuwa watu hufanya mambo wakiwa na matarajio kuwa mitazamo ya umma kuwahusu itaheshimiwa kwa kawaida kila mtu atatarajiwa kuheshimu mahitaji ya uso wa mwingine, kwa hivyo naye anaunga mkono hoja kuwa kuna njia nyingi za kutekeleza vitendo vya kuokoa uso.

### 1.8.4 Mikakati ya kuheshimu nyuso

Katika kipengele hiki, Brown na Levinson (1978) wanasema kuwa kila mwanadamu katika jamii ana uso ambao angependa uheshimiwe, na pia angetaka uso wa watu wengine uheshimiwe. Katika harakati za shughuli mbalimbali katika jamii, kuna mambo mawili yanayoweza kufanyika kwa uso:

a) Kuheshimiwa

b) Kudhurika

Katika mazungumzo au mawasiliano, kuheshimiwa kunaweza kutokea kwa mzungumzaji au msikilizaji Brown na Levinson (1978) wanasema kuna baadhi ya matendo hutishia uso (Face Threaning Acts) Kunayo mazungumzo yanayoweza kuvuruga uso chanya wa msemaji kwa kukosea matakwa ya msikilizaji. Hali kadhalika mazungumzo mengine yanaweza kuvuruga uso chanya kutokana na msemaji kutojali hisia zinazompata msikilizaji. Wanadai kwamba mazungumzo yanahusiana zaidi na kuchunguza matarajio ya upole yanayolenga uso kwa ujumbe unaotolewa. Ni kutokana na madai haya ndipo dhana ya upole chanya na upole hasi ulijitokeza nazo ndizo zilikuwa ni mikakati ya kuheshimu nyuso pamoja na makakati wa rekodi. (record strategy).

### 1.8.5 Upole chanya

Hudhamiria kupunguza Tishio la uso chanya wa msikilizaji au anayezungumziwa. Hujihusisha na umoja wa mzungumzaji na msikilizaji kuonyesha wanataka kitu kimoja. Hutumiwa ili kumfanya msikilizaji afurahie hali yake, mahitaji yake na wakati mwingi hutumika katika hali ambapo hadhira inafahamiana vizuri na mzungumzaji. Upole chanya vilevile uhusisha kuzungukazunguka na kujaribu kuzuia migongano, umoja, kupeana sifa na kuwepo na uneni wa kirafiki, na kijumla upole chanya unahusika na uso chanya wa watu. Mifano ya upole chanya ni kama vile;

- kutoa ahadi au kitu kwa mfano; "ukifika mapema kesho nitakupa zawadi."
- kuzua mzaha katika mazungumzo mfano; Lo! Maria umerembeka kweli! unaonekana kama malkia.
- Uhusisha mzungumzaji na msikilizaji katika shughuli fulani. Mfano: iwapo tutapika chakula hiki vizuri, wananuzi wataifurahia.
- Mtu kuwa na matumaini mema. Mfano; Nitakununulia baiskeli mwezi ujao nikiongezwa mshahara.
- Huzingatia mahitaji ya msikilizaji wake. Mfano; Leo umekimia sana, kuna shida gani?
- Kuzuia kutoafikiana kwa jambo. Mfano: chai yenyewe ni kizuri sana, japo sukari imezidi.
- Kuzidisha au kutia chumvi kwa faida ya msikilizaji. Mfano: Lo! umejikwatua kwatu kwatu! kwani unaenda kwenye kasri kukutana na mfalme.

### 1.8.6 Upole hasi

Hudhamiria kwamba lazima mtu aingiliane na watu wengine na aombe watu wengine. Lazima kutafuta mbinu ya kuokoa uso hasi ili usidhuru watu wengine. Katika mkakati huu, uwezekano

wa kudhuru hisia za hadhira ni mwingi. Kuwa na uso hasi kunatokana na mtu kutaka kuwa huru. Hivyo basi kuomba kitu kutoka kwa hadhira bila kujali uso hasi wa hadhira huenda kukaikosesha amani. Mzungumzaji anapotambua kuwa hadhira inahitaji uhuru wake hutumia mkakati wa upole hasi.

Brown na Levinson wanatoa mifano ya upole hasi kama ifuatavyo:

- kutumia njia za mzunguko / maswali, mfano; Huenda Mariamu atampa leo au unaweza kuniletea hela hizo kesho?
- Madanganyo ya upole; mfano: Tumekukosa sana, utarudi lini?
- Usiwe dhahiri; mfano; Je umeona aliyechukua kalamu yangu ?
- Matumizi ya tasfida (matumizi ya maneno ya adabu yakwepayo miiko lugha); mfano: Juma ana mkono mrefu (kumaanisha ni mwizi).
- Kutumia pronauni za wingi; mfano – wanahofia hawatapata mavuno ya kutosha mwaka huu.

Carter na McCarthy (1994) wamekubaliana nao Brown na Levinson katika maelezo yao kuhusiana na upole hasi unapoelezewa kama utafutaji wa hisani au mzungumzaji kuomba msikilizaji hisani. Huu ni mfano uliodhahiri wa mkakati hasi ya upole inayotumika.

### 1.8.7 Mkakati wa rekodi

Mkakati wa rekodi ni wa namna mbili.

a) Kuwa kwenye rekodi

b) Kuwa nje ya rekodi

### 1.8.8 Kuwa kwenye rekodi

Mkakati huu kwa kawaida huwa haujaribu kupunguza tishio la uso wa msikilizaji ingawa kuna njia ambapo upole wa kuwa kwenye rekodi hutumiwa ili kujaribu kupunguza uthabiti wa Tendo la kutishia uso. Kwa kawaida mkakati huu hutumiwa na wazungumzaji walio na ushirikiano mzuri na wa karibu na hadhira yao. Ushirikiano huu unaweza kuwa kati ya watu wa familia au hata marafiki wa karibu. Katika kutumia mkakati huu, kuna uwezekano wa kusema mambo moja kwa moja kwa hadhira, na hali hii huenda ikadhuru uso hasi wa hadhira. Brown na Levinson walidokeza matukio kadhaa ambapo mkakati wa kuwa kwenye rekodi unaweza ukatumika. Kwa mfano;

- Kumkaribisha mtu; mfano: - Ingia, Karibu ndani.
- Pendekeza jambo au toa kitu. Mfano; kula! Acha hizo vyombo nitaosha mwenyewe.
- Kuwepo au kutokuwepo na haja ya kuudumisha uso wa mtu; mfano; usisahau kuosha blanketi leo!
- Kuzungumza kana kwamba ustadi mkubwa sana unahitajika. Mfano: Nitazame wewe!
- Hali ambapo kupunguza kwa tishio hakutokei
- Pale utekelezaji wa Tendo la kutishia uso linamfaidi msikilizaji mfano; Eh dada, zipu yako....

### 1.8.9 Kuwa nje ya rekodi

Mkakati wa kuwa nje ya rekodi ni mkakati usiokuwa wa dhahiri. Hutumia lugha isiyo ya moja kwa moja, ambapo mzungumzaji hutumia njia ya mzunguko na kuwa katika hali ya kutolazimisha jambo. Mzungumzaji huteua maneno yasiyo ya moja kwa moja na kuyatumia kupitishia ujumbe wake kwa hadhira, na hadhira ikaelewa na kufanya atakavyo pasipo kuhisi

kuingiliwa uso hasi: mzungumzaji anaweza kutumia njia ya mzunguko kwa msikilizaji wake kwa kusema hivi;

"Tangu jana asubuhi sijala chochote."

Maelezo yaliyofichwa hapa ni kuwa, msemaji anahisi njaa na anauliza kama kuna uwezekano na kupewa chochote cha kula, bila kuuliza waziwazi aandaliwe chakula. Wakati mwingine mtu hutenda matendo fulani ili hadhira imfanyie anavyotoka.

Kipengele hiki cha kuheshimu nyuso za watu ni mbinu mojawapo ambayo imetumiwa na wasanii kama Munishi katika baadhi ya nyimbo zake. Nyimbo hizo zimewasilishwa kwa kutumia mkakati wa upole. Kuokoa nyuso za wasikilizaji na jamii yote kwa jumla.

Tulichagua nadharia hii ya upole ili kuchanganua nyimbo teule za dini zilizoimbwa na Munishi kwani nyimbo hizo zina mawaidha kwa jamii, na mawaidha hayo yamewasilishwa kwa njia ya mafumbo, tasfida na mbinu zingine za lugha. Mafumbo hayo yanaweza tu kufumbuliwa baada ya hadhira au msikilizaji kutathmini jamii lugha pamoja na matukio katika mazingira wanamokaa au kuishi.

Mwimbaji wa nyimbo hizi ametumia usemii katika kuwasilisha ujumbe wake. Nadharia ya kitendo usemi (Speech Act Theory) huonyesha vile tunavyotenda mambo kadhaa kupitia usemi. Nadharia ya kitendo usemi ilianzishwa na mwanafalsafa J.L. Austin miaka ya 1930 na kuchapishwa katika kitabu chake "*How to do things with words*" (1962). Kwa mujibu wa Austin, lugha hutumika kutenda mambo kadha wa kadha kama vile kuonya, kuahidi, kulaumu, kushukuru, n.k. Hivi vyote ni vitendo vya usemi. Maoni ya Austin ni kuwa, lugha ya binadamu huwasilisha maana kupitia utendaji (performance), mzungumzaji huweza kutamka maneno fulani

ambayo huwasilisha ujumbe fulani. Hata hivyo hatukutazama nadharia hii ya Austin kiundani kwa vile tulitumia nadharia ya upole.

Nadharia hiyo ilitusaidia kuweka suala la upole wazi kwani uzungumzi hutumika kutekeleza jambo fulani kwa kutumia maneno, hivyo majukumu fulani katika jamii hutekelezwa kupitia nyimbo zinazoimbwa na wanasanii tofauti.

Katika kuchanganua nyimbo teule za Munishi, mwimbaji huyo ametumia usemi na utendaji katika kutoa tahadhari kwa jamii huku akizingatia mkakati wa upole ya kuokoa uso.

## 1.9 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA.

Tahakiki nyingi sana zimeandikwa katika fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo, tahakiki hizi zimejikita katika fasihi andishi. Kufikia sasa, fasihi andishi ya Kiswahili imepata kazi nyingi sana na hivyo imekuwa kwa kiwango cha juu zaidi. Riwaya, tamthilia, hadithi fupi na mashairi yamechapishwa kwa upande mwingine, fasihi simulizi imebakia nyuma.

Taban Lo Liyong akinukuliwa na Nandwa na Bukenya (1983) akizungumzia Fasihi simulizi ya Kiafrika kama nyanja tasa kwa sababu haijafanyiwa utafiti wa kuridhisha ambao unaweza kuikuza na kuleta welewa zaidi kuihusu. Hata hivyo, katika miaka ya sasa, wasomi pamoja na watafiti wamejitokeza kushughulikia nyanja hii ya fasihi. Miongoni mwa watafiti waliofanya tafiti za hivi karibuni ni pamoja na Kineene wa Mutiso (1985), Timammy (2002), Olali (2004) na wengine ambao wameonyesha umuhimu wa fasihi hasa utanzu wa nyimbo katika tafiti zao. Walichangia katika kudhihirisha kuwa fasihi si kazi ya wale ambao hawatumii akili zao kama asemavyo Finnegan (1970). Timammy (2002) alijikita katika utanzu wa nyimbo ambapo

alishughulikia nyimbo za harusi za jamii ya Waswahili na kuweka bayana umuhimu wa fasihi simulizi katika jamii za kiafrika haswa nyimbo za kitamaduni.

Wataalamu kadhaa wametoa maana mbalimbali kuhusu nyimbo kulingana na kamusi sanifu ya Kiswahili (Tuki: 1981) wimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki.

Mulokozi (1987) anasema kuwa wimbo ni kile kinachoimbwa. Naye Matteru (1981), katika makala yake 'Fasihi simulizi na uandishi' anasema kwamba nyimbo ni aina ya ushairi unaoimbwa pekee au kwa kuhusishwa na ngoma au pia kwa kuchezwa na mwimbaji wake. Pia anadokeza kuwa nyimbo ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi, melodia, mapigo na muwala. Wimbo unaweza kuimbwa na mtu mmoja pekee au na wazumi wake wakiitikia mikarara, vilevile, nyimbo zina mfuatano au mpangilio maalum wa sauti, mwendo, picha au ishara. Naye Thonya (1978) anakubaliana na maoni ya Matteru (K.H.J) anaposema kwamba wimbo ni aina ya ushairi uliotiwa sauti na uliokusudiwa kuimbwa na kuleta maana ya ujumbe kwa jamii. Hoja hilo ni kweli hasa katika utafiti wetu ambapo mwimbaji ametumia lugha kwa kurejelea mikakati ya upole kuwasilisha ujumbe wake kwa jamii.

Freuchen (1962) kama anavyonukuliwa na Finnegan (1970) katika kufafanua maelezo ya nyimbo anasema kuwa nyimbo ni mawazo yanayoimbwa na watu baada ya kusukumwa na nguvu maalum. Mawazo haya hayawezi kutolewa kwa hadhira katika mazungumzo ya kawaida yakaeleweka ama kuleta athari iliyokusudiwa. mawazo ya mwanadamu yanasukumwa na nguvu maalum iliyozingirwa wakati huo kama vile furaha, hofu, uchungu au utulivu.

Mawazo yakimfurika mtu kichwa, huenda akapoteza fahamu au kuwa katika hali ya wasiwasi, hivyo kuathirika kwa namna fulani, na kunakuwa na matukio mapya, maneno yatakayohitajika katika kulieleza tukio hilo jipya yatajitokeza yenyewe, na maneno hayo ndiyo yatakayounda wimbo.

Nyimbo ni aina ya tanzu za fasihi simulizi. Fasihi simulizi ni sanaa ambayo hutumia lugha, hasa maneno ambayo yametamkwa kupitia kinywa cha binadamu. Fasihi simulizi ni mali ya jamii yenye manufaa mengi sana kwa binadamu, na binadamu kupitia uwezo wake wa kutamka maneno, huwasilisha ujumbe kwa njia ya mazungumzo, kughani, uimbaji na kutongolewa hadithi. Hivyo fasihi simulizi huweza kueleza hisia za binadamu kama vile furaha, kero, matarajio, uzito wa fikira na hata matumaini yake, pia huelezea imani, mila na hali tofauti maishani.

Nyimbo zapaswa kuwa na mpangilio maalumu, na zinapoimbwa hutumia vipengele vingi katika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwa hadhira lengwa, vipengele hivi ni pamoja na vidokezo, miguno, milio, toni, vituo, kiimbo, kimya, kasi na kadhalika.

Kulingana na tafiti zilizofanywa hapo awali, nyimbo tofauti huwa na ujumbe tofauti kwa hadhira, na nyimbo hizo hujikita katika kutoa mafundisho ya hekima, maonyo, maadili, malezi na busara za wahenga. Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa inabainika kwamba nyimbo ni fani ya fasihi simulizi. Fani hii hutolewa katika muktadha fulani ili maana ieleweke. Inabainika kuwa maelezo haya basi yanatutolea msingi thabiti ya kuchanganua nyimbo mbili za dini zilizoimbwa na msanii Foustin Munishi. Inadhihirika kwamba ili kuelewa vyema matini ya

nyimbo ni lazima ziimbwe na kwa muwala fulani. Mulokozi (1981) alitoa sifa kadhaa za nyimbo kama ifuatavyo ;

i) Muziki wa sauti ya mwimbaji

ii) Muziki wa ala

iii) Matini au maneno yanayoimbwa

iv) Hadhira inayoimbiwa.

v) Muktadha uliofungamana na wimbo huo. Kwa mfano ; ibada ; sherehe, kilio, n.k.

Freuchen (1962) akinukuliwa na Finnegan anaunga mkono mawazo haya kwa kusisitiza kwamba, kazi ya kisanaa ya nyimbo hutokana na mazingira. Mazingira ndiyo yanazalishwa kwa hadhira husika kwa njia ya sauti.

Wimbo ni tungo la Kishairi linaloimbwa kwa muwala fulani. Ala za muziki zinazotumika huchukua kipao mbele zaidi ya maneno katika wimbo huo, tofauti na shairi ambapo maneno huchukua kipao mbele. Kulingana na mayhead (1965) umaarufu wa muziki katika wimbo huruhusu maana ya maneno kuchukuliwa sawa na uimbaji wa muziki.

Beja (2000) anasema kwamba huwa inachukuliwa kuwa maana ya maneno katika wimbo, na yaliyomo hubeba ujumbe ambao huongoza kuridhika kwa msikilizaji au hadhira inayosikiliza ujumbe huo. Hali kadhalika, anaongezea kuwa mbinu za lugha zinazotumika katika nyimbo huzipa mvutio fulani ambayo huvutia hadhira na kuwafanya kuridhika kusikiliza nyimbo hizo. Tunakubaliana na Timammy (2002 : 208) anaposema kuwa pana haja ya kufanya utafiti finyu ili kupata lugha ya nyimbo.

Finnegan (1970) alifanya utafiti kuonyesha umuhimu wa nyimbo katika jamii za kiafrika na jinsi dhima za nyimbo hizo zinavyobainika. Utafiti wake uliweka wazi ukweli kwamba, umuhimu wa nyimbo hupatikana kupitia maudhui na mtindo. utafiti wa Finnegan ulikuwa muhimu kwa utafiti wetu kwani ulihusu mtindo katika nyimbo, ambapo kipengele hiki hurejelea pia lugha.

Ngugi (1986) anasema kwamba nyimbo huwa zinathibitisha ubunifu wa mtu pamoja na uwezo wa kutumia akili yake kwa urazini. Nyimbo huonyesha maswala muhimu kuhusu jamii. Jukumu la nyimbo haswa ni kuielimisha jamii kupitia onyo, kuifahamisha, pamoja na kuitahadharisha kuhusu hatari iliyoko maishani. Jukumu hili hutekelezwa kupitia maudhui yashirikishwayo katika nyimbo hizi : utafiti wa Ngugi (K.H.J.) ulichangia sana utafiti huu kwani katika kushughulikia maudhui pia kuna kipengee cha kutahadharisha jamii kuhusu hatari iliyoko maishani katika utafiti huu wetu, tukirejelea wimbo – 'maji yana mdudu'; msanii anatumia lugha kwa upole ili kuokoa uso wa msikilizaji kwa njia ya kuwatahadharisha hadhira yake. Anahimiza wanajamii kuwa wanywe maji kutoka visima vyao wenyewe. Tahadhari hii ni kutokana na matukio yaliyomo katika jamii hii leo, na ukosefu wa maadili ndio imeleta kuwepo kwa janga ambalo halina suluhu.

Nkonge (1988) alitafiti fani na maudhui katika nyimbo za Joseph Kamaru ambapo alijaribu kuonyesha jinsi Kamaru anavyochota maudhui yake kutoka matukio ya kijamii na yale ya kisiasa nchini Kenya. Utafiti wake ulikuwa wa manufaa kwa utafiti huu kwani ulidhihirisha kwamba kabla msanii kuimba huwa anachota malighafi yake kutoka kwa matukio ya kijamii – matukio hayo huenda yanalenga watu walio kwenye ndoa, vijana, wazee au watu katika daraja tofauti katika jamii.

Rapando (1991) katika utafiti wake alisawiri nyimbo kama zao la miktadha ya kijamii. Nyimbo hizi huibuka kufuatia utaratibu fulani ambao unachangiwa na maswala ibuka katika jamii. Tukirejelea utafiti wetu, tunaona kuwa msanii wa nyimbo tunazochanganua alilenga jamii kutokana na matukio yaliyomo sasa. Kule kupotoka kwa watu na kupoteza maadili kiasi cha kuingilia ndoa ya wengine kwa kuwa na macho ya nje, kulimfanya msanii kuona haja ya kutoa tahadhari kwa jamii kupitia wimbo, aliyoimba akitumia mkakati wa upole ili kuokoa uso.

Kingei (1993) walifanya utafiti kuhusu umuhimu wa nyimbo za taarab nchini Kenya kati ya 1963 na 1990. Alichunguza utendakazi wa nyimbo hizo kwa kuzingatia lugha, utamaduni, mawasiliano pamoja na maudhui ya nyimbo hizi. Utafiti wa Kingei ulitusaidia kubaini mambo muhimu ya kuzingatia katika kuchanganua nyimbo. Ingawa utafiti huo ulikuwa tofauti, lakini ilitufaa katika kutambua namna msanii alivyotumia lugha, na ni kwanini ? Hivyo, nadharia ya upole ikawa ndio mwafaka zaidi katika kuchanganua nyimbo hizi teule.

Mbiti (2001) anasema kwamba nyimbo, methali, hekaya na hadithi zapatikana katika jamii nyingi za Kiafrika. Fani hizi huwa zinatokea katika kipindi maalumu na huwa na ujumbe unaobainika katika kipindi hicho. Maoni ya Mbiti (k.h.j) yalitunufaisha katika utafiti huu kwani yalifafanua kuwa nyimbo hutokea katika kipindi fulani maalum. Nyimbo tunazochanganua kwa wakati huu, yalitungwa kwa wakati maalum kutokana na matukio katika jamii. Matukio hayo yalielekeza msanii kutunga nyimbo za kuwatahadharisha wanajamii kuhusu mienendo yao. Alifanya hivyo kwa kutumia mikakati ya upole ili kuokoa uso wa msikilizaji na jamii kwa jumla.

## 1.10 MBINU ZA UTAFITI

Utafiti wetu umejikita maktabani.

### 1.10.1 Eneo la Utafiti

Tulipata matini mbalimbali ya nyimbo za Munishi kutoka kwenye mtandao na kwenye kanda zake alizoimba na kurekodi. Baada ya kukusanya data tutakayohitaji tulizichanganua nyimbo mbili tulizoziteua : wimbo wa maji yana mdudu na wimbo wa malebo. Tulichagua nyimbo hizi kwa sababu nyimbo zote za kidini huwa na maudhui na mitindo iliyofanana kwa hivyo nyimbo hizi mbili zinawakilisha nyimbo zote za kidini. Pia muda wa kufanya utafiti ni mchache kuweza kushughulikia nyimbo zote za kidini. Pia tulichagua matini haya kutokana na sifa yake ya upole kama inavyojidhihirisha katika matumizi ya lugha na mtindo.

Nyimbo hizi zilichaguliwa kulingana na umaarufu wake katika nyimbo za kidini. Nyimbo ambazo huimbwa sana katika makanisa na ambazo zimeimbwa kwa miongo mingi ndizo zilizochaguliwa kuwakilisha nyingine. Hii ni kwa sababu ya muda wa utafiti ambao haungetosheleza kushughulikia nyimbo zote.

### 1.10.2 Sampuli

Sampuli yetu imetoka katika nyimbo za kidini hasa nyimbo mbili za msanii Munishi. Sampuli tuliyotumia ilikuwa sampuli lengwa (purposive sampling). Nyimbo za kidini ni nyingi lakini tulichagua nyimbo mbili za Munishi ambazo zimeimbwa kwa muda mrefu na visasi vingi. Nimbo zingine za kidini zina mitindo maudhui yanayofanana na hizi nyimbo mbili teule za Munishi. Kwa hivyo nyimbo hizi teule zimewakilisha zote za kidini

### 1.10.3 Nyenzo za Utafiti

Tulitumia nyenzo zilizohitajika kupata data tuliyohitaji. Tulisikiliza nyimbo kutoka kwa kanda za Munishi. Nakala za nyimbo mbili za munishi zilitusaidia kuelewa mambo kuhusu kupokelewa kwa nyimbo hizi.

## 1.11 UCHANGANUZI WA DATA

Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa misingi ya nadharia ya upole. Tulitathmini suala la upole kwenye matini teule ya nyimbo mbili za msanii Munishi kwa kuongozwa na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987). Katika uchanganuzi, tulichanganua maneno katika nyimbo na kuchunguza athari zake kwa nyuso za wanaohusika. Baada ya kuchanganua nyimbo tuliweza kuthibitisha kuwa kuna mikakati ya koukoa nyuso za wanaohusika kwenye matini teule ya nyimbo mbili za Munishi.

## 1.12 UMUHIMU WA UTAFITI

Katika kuchanganua nyimbo teule za Munishi, utafiti huu utaonyesha umuhimu kwa wasanii, wanaisimu na hata watafiti wengine. Kwa Wasanii, wakisoma kazi hii watatambua umuhimu wa kuzingatia upole wanapoimba nyimbo zao, na kuwasilisha ujumbe kwa hadhira.

Wanaisimu watakuwa na msingi wa kutafiti zaidi nyimbo ambazo zimeimbwa na wasanii waliozingatia mikakati ya upole katika kuwasilisha ujumbe wao.

Watafiti wengine wanaweza kuvutiwa kutalii nyimbo ambazo hazijatumia mikakati ya upole, na kutaka kujua sababu za waimbaji hao. Kukiuka dhana ya upole katika kazi zao. Hivyo basi ni dhahiri kuwa utafiti huu utawatia motisha watu tofauti katika jamii kuona umuhimu wa kutumia

mikakati ya upole katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira tofauti na hata katika mawasiliano miongoni mwa watu katika jamii.

## 1.13 HITIMISHO

Nyimbo zimekuwa sehemu muhimu sana ya fasihi tangu jadi. Aghalabu kila jamii ina nyimbo zake ambazo hutumiwa kuwasilisha ujumbe fulani kwa jamii. Nyimbo ni sehemu ya utamaduni. Jinsi utamaduni wa jamii fulani ulivyo mpana, ndivyo utamaduni huo ulivyo na nyimbo nyingi. Nyimbo zimetungwa kuhusu kila nyanja ya maisha, ambapo kuna nyimbo kuhusu ndoa, mapenzi, shughuli za Kilimo, dini, kifo na kadhalika.

## SURA YA PILI

## NYIMBO; AINA NA MAJUKUMU.

### 2.0 UTANGULIZI

Katika sura ya kwanza, tuliangazia mambo ya kimsingi kuhusu utafiti wetu. Katika sura hii, tumeangazia kwa undani maana ya nyimbo, aina za nyimbo, majukumu ya nyimbo na vipengele vya kimuktadha katika nyimbo. Kwa kuwa aina za nyimbo ni nyingi, hatukuweza kushughulikia zote bali baadhi yazo. Suala la upole katika matini teule ya nyimbo za Munishi yataeleweka vizuri baada ya kujiuliza maswali haya;

1. Je wimbo ni nini?
2. Wimbo huimbwa wapi?
3. Wimbo huimbwa na kina nani?
4. Je, kuna aina zipi za nyimbo?
5. Je, nyimbo zina majukumu gani katika jamii?
6. Je, Munishi alitumia mtindo gani katika nyimbo mbili teule?

Vipengele hivi ni muhimu kuangaziwa kwani nyimbo zote hutofautiana na huimbwa kwa madhumuni mbalimbali katika jamii. Umuhimu wa sura hii ni kuwa inauwekea msingi zaidi utafiti wetu.

### 2.1 NYIMBO

Wataalamu mbalimbali wametoa maelezo mbalimbali kuhusu maana ya nyimbo. Kulingana na kamusi ya Kiswahili Sanifu(TUKI 1981) wimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki. Naye M'Ngaruthi(2008) anasema nyimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya kuvutia na

kwa mahadhi ya kupendeza. Inabainika wazi kuwa nyimbo zimekuwemo miongoni mwa binadamu hata kabla ya maandishi kuvumbuliwa na imekuwa ni mojawapo wa njia za watu kujitumbuiza katika sherehe mbalimbali ambapo yaaminika binadamu asiyevutika na wimbo au mdundo wa aina yoyote ana kasoro kubwa. Nyimbo vilevile hutumiwa kupitisha ujumbe kwa watu wenye umri tofauti katika jamii. Vilevile, Matteru (1981), katika makala yake, 'Fasihi simulizi na andishi' anasema kwamba nyimbo ni aina ya ushairi unaoimbwa pekee au kwa kuhusishwa na ngoma au pia kwa kuchezwa na mwimbaji wake. Pia anadokeza kuwa nyimbo ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi, melodia, mapigo na muwala. Wimbo unaweza kuimbwa na mtu mmoja pekee au na wazumi wake wakiitikia mikarara. Vilevile, nyimbo zina mfuatano au mpangilio maalum wa sauti, mwendo, picha au ishara.

Thonya(1978) anasema kwamba wimbo ni aina ya ushairi uliotiwa sauti na uliokusudiwa kuimbwa na kuleta maana ya ujumbe kwa jamii.

Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, inabainika kwamba nyimbo ni fani ya fasihi simulizi. Fani hii hutolewa katika muktadha fulani ili maana ieleweke. Inabainika kuwa maelezo haya basi yanatutolea msingi thabiti wa kuchanganua nyimbo mbili za dini zilizoimbwa na msanii Foustin Munishi. Inadhihirika kwamba ili kuelewa vyema matini ya nyimbo ni lazima ziimbwe na kwa muwala fulani. Mulokozi (1981) anasema kwamba wimbo ni kile kinachoimbwa. Alitoa sifa kadha za nyimbo kama ifuatavyo:

i) Muziki wa sauti ya mwimbaji.

ii) Muziki wa ala.

iii) Matini au maneno yanayoimbwa.

iv) Hadhira inayoimbiwa.

v) Muktadha uliofungamana na wimbo huo kwa mfano; ibada, sherehe, kilio, n.k.

Freuchen (1962) akinukuliwa na Finnegan anaunga mkono mawazo hayo kwa kusisitiza kwamba, kazi ya kisanaa ya nyimbo hutokana na mazingira. Mazingira ndiyo yanazalisha hisia na hatimaye mawazo kwa msanii wa nyimbo ili aweze kufanya kazi yake ya usanii. Hivyo basi, katika nyimbo, panapaswa kuwa na wazo maalum ambalo linawasilishwa kwa hadhira husika kwa njia ya sauti.

Wimbo ni tungo la kishairi linaloimbwa kwa muwala fulani. Ala za muziki zinazotumika huchukua kipaumbele zaidi ya maneno katika wimbo huo, tofauti na shairi ambapo maneno huchukua kipaumbele. Kulingana na Mayhead (1965) umaarufu wa muziki katika wimbo huruhusu maana ya maneno kuchukuliwa sawa na umbaji wa miziki. Nyimbo ni zao la shughuli za binadamu pamoja na hisia zake na hivyo huzingatia miktadha mbalimbali. Nyimbo huwa zimefungamanishwa na muktadha fulani pale ambapo pana hadhira na matini. Hadhira huwa ni wale wanaosikiliza au kuzitazama nyimbo hizi, nayo matini yakiwa ni yale matamshi yenyewe kwa njia ya uimbaji.

Nyimbo ni aina ya tanzu za fasihi simulizi. Fasihi simulizi ni sanaa ambayo hutumia lugha, hasa maneno ambayo yametamkwa kupitia kinywa cha binadamu. Fasihi simulizi ni mali ya jamii yenye manufaa mengi sana kwa binadamu, na kupitia uwezo wake wa kutamka maneno huwasilisha ujumbe kwa njia ya mazungumzo, kughani, kuimba na kutongolewa hadithi. Hivyo, fasihi simulizi huweza kueleza hisia za binadamu kama vile furaha, kero, matarajio, uzito wa fikira na hata matumaini yake. Pia hueleza imani, mila na hali tofauti maishani. Nyimbo zapaswa kuwa na mpangilio maalum, na zinapoimbwa hutumia vipengele vingi katika kufanikisha

uwasilishaji wa ujumbe kwa hadhira lengwa. Vipengele hivi ni pamoja na vidokezo, miguno, milio, toni, vituo, kiimbo, kimya, kasi na kadhalika.

Kulingana na tafiti zilizofanywa hapo awali, nyimbo tofauti huwa na ujumbe tofauti kwa hadhira, na nyimbo hizo hujikita katika kutoa mafundisho ya hekima, maonyo, maadili, malezi na busara za wahenga.

## 2.2 AINA ZA NYIMBO

Takribani jamii zote za waafrika zilikuwa na nyimbo ambazo maudhui yake yaliegemea ushindi wa kazi, ushindi wa vita, mafanikio, matarajio, matumaini, maadili, malezi na takriban shughuli zote za binadamu. Katika sehemu hii, tutaziangalia kwa mujibu wa hatua mbalimbali za maisha ya binadamu tangu kuzaliwa kwake hadi kufa. Kutokana na haya, Mulokozi (1989) aliziweka nyimbo katika makundi mbalimbali kama yalivyo hapa chini.

i) Nyimbo za kuongoa watoto(bembelezi)

ii) Nyimbo za sherehe ya kuzaliwa mtoto.

iii) Nyimbo za kumpa mtoto jina.

iv) Nyimbo za dini.

v) Nyimbo za nyiso/ tohara(jando na unyago).

vi) Nyimbo za watoto.

vii) Nyimbo za harusi.

viii) Nyimbo za mapenzi.

ix) Nyimbo za kazi (Hodiya).

x) Nyimbo za mayanga (mbolezi).

xi) Nyimbo za kizalendo.

xii) Nyimbo za tambiko.

xiii) Nyimbo za kishujaa.

Nyimbo zote zilikuwa na waimbaji na hadhira tofauti na ziliimbwa nyakati tofauti kwani baadhi yake ziliongozwa na matukio, maadili na miiko fulani. Lugha iliyotumika ilikuwa ya kitamathali na hata msamiati ulitegemea fanani/msanii na hadhira. Kwa mfano, msamiati uliotumika na watoto ni tofauti na ule wa watu wazima. Msamiati huu uliteuliwa kwa kuzingatia uokoaji wa nyuso mbalimbali za wanaohusika.

## 2.3 MAJUKUMU YA NYIMBO NA VIPENGELE VYA KIMUKTADHA

Katika utamaduni wa kiafrika, nyimbo zilipamba sherehe na tamasha mbalimbali na zingali zinafanya hivyo. Nyimbo ni zao la shughuli za binadamu pamoja na hisia zake na hivyo huzingatia miktadha tofauti. Nyimbo hizi huwa na maudhui na mitindo yake inayohusiana na shughuli inayotekelezwa. Maudhui na mitindo hii hubadilika na wakati pale ambapo husawiri historia ya wakati na mwelekeo wa jamii. Nyimbo kama asemavyo Wamitila (2003) zinatekeleza majukumu muhimu katika maisha ya kila siku. Maadili yalikuzwa na hata sasa yanakuzwa kwa kupitia nyimbo na miongoni mwa jamii mbalimbali.

Licha ya ukuwaji wa maadili na kuacha mila miongoni mwa vizazi vya leo, nyimbo huchangia katika kujaribu kuwaelimisha wanajamii umuhimu wa kuwa na maadili. Nyimbo hutekeleza majukumu muhimu ya kushauri, kuonya, kukejeli, kutia moyo, kuelimisha, kuburudisha, kukashifu na kubeza. Basi, kwa kubainisha majukumu haya, tutaelezea nafasi ya aina tofauti za nyimbo katika jamii.

### 2.3.1 Nyimbo za sherehe ya kuzaliwa

M'Ngaruthi (2008) anasema kuwa kuzaliwa kwa mtoto kulichukuliwa kama tukio muhimu sana katika jamii kwani ilidhihirisha kupanuka kwa jamii hiyo, hasa nyakati zile ambazo watoto waliangamizwa sana na maradhi na utapia mlo. Katika jamii za kiafrika, kuzaliwa kwa mtoto wa kiume ilichukuliwa au kupokelewa kwa furaha zaidi kuliko mtoto wa kike alipozaliwa. Kwa mfano, katika jamii ya Wameru, mtoto wa kiume alipozaliwa alikaribishwa kwa vigelegele vinne huku wa kike akipokea vitatu.

### 2 3.2 Nyimbo za kumpa mtoto jina

Jamii tofauti ziliwapa watoto majina kulingana na jinsia ya mtoto huyo. Kuna jamii zilizotumia misimu tofauti kuwapa watoto majina, wengine walipata majina kutegemea majira ya siku au mwaka. Jamii zingine zilitumia wakati, ambapo mtoto angetajwa kulingana na wakati alipozaliwa, ingawa tofauti ingebainika kwa herufi za kwanza za jina hilo kama Otieno( mvulana aliyezaliwa usiku), Atieno (msichana aliyezaliwa usiku), Wafula(mvulana aliyezaliwa msimu wa mvua) na Nafula(msichana aliyezaliwa msimu wa mvua).

Kuna jamii zilizowapa watoto majina ya wanyama au miti, iwapo watoto waliotangulia walikuwa wamefariki. Jamii kama ya Agikuyu walipeana majina kwa watoto wao kutokana na babu, nyanya, mjomba, au shangazi. Nyimbo zilizotungwa na kuimbwa katika sherehe hizi ziliwasifu watu waliotajwa.

### 2.3.3. Bembelezi/ Bembe/ Bembezi

Nyimbo za bembelezi zilikuwa ni za kuongoa mtoto kuonyesha hali ya kumjali na kumfanya apate kulala. Mtoto hangeachiliwa kulia ovyo kwani ilichukuliwa kuwa ishara ya kutojali au

malezi mabaya. Hali hiyo ya kutojali ingemfnya mama wa mtoto huyo kukaripiwa na hata kutengwa na wanawake wengine katika shughuli za kijamii. Nyimbo hizi huwa hazina maneno maalum, hutegemea mwimbaji, mahali, tukio, umri wa mtoto au jinsia yake.

### 2.3.4 Nyimbo za dini

Hizi ni nyimbo zilizo na uhusiano na Mungu au miungu. Misingi yao huwa ni ya dini za kienyeji au zile za kimagharibi. Nyimbo hizi zinaweza kuimbwa na mtu binafsi au makundi ya watu, ambapo ujumbe hutegemea matukio yaliyopita, yaliyopo au yajayo katika siku za usoni. Nyimbo hizi hunuiwa kuwashauri watu katika jamii, kuwahimiza, kuonya, au kuwapa watu moyo baada ya matatizo fulani kutokea. Mwimbaji anaweza kutumia lugha kwa ufundi akirejelea tamathali za usemi, methali, mafumbo na hata semi tofauti katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira tofauti. Nyimbo za dini pia hutumika wakati watu wanataka kujinyenyekeza mbele ya Mungu. Nyimbo hizi huimbwa kwa miktadha mingi na waimbaji na hadhira yake hutofautiana, hasa namna wanavyowasilisha ujumbe wao. Kwa mfano; Jinsi watakavyoimba watoto wafuasi wa dini ya kiislamu katika madrassa sivyo watakavyoimba watoto wafuasi wa dhehebu la sabato.

Nyimbo za injili pia ni sehemu ya nyimbo za dini na hufanya majukumu sawa na nyimbo za kidini.

### 2.3.5. Nyimbo za nyiso/ tohara

Jamii nyingi za kiafrika zilithamini tohara za wavulana na wasichana, ambapo wavulana walikuwa jandoni ilhali wasichana unyagoni. Kwa wakati wa sasa, tohara kwa wasichana imekuwa kinyume cha sheria na pia inasababisha madhara kwa wasichana hasa wanapotimia utu uzima, hivyo haipo. Tohara ilithaminiwa na makabila yote ya kibantu na mengine ya kinailotiki

kama vile Kikalenjini, Maasai, Samburu na kadhalika. Jamii ilisisitiza ifanywe kijijini, hivyo wale waliotahiriwa hospitalini walidharauliwa na kutengwa. Nyimbo za tohara ziliimbwa kwa malengo tofauti kama vile;

i) Kuwakusanya pamoja na kuwapa moyo watahiriwa.

ii) Kuukejeli uoga/waoga.

iii) Kuuaga utoto kirasmi.

iv) Kuwatayarisha watahiriwa ki-hisia ili kukabiliana na kisu kijasiri.

v) Kushangilia au kufurahia hatua ya kutoka utotoni hadi utu uzimani.

vi) Kuwatayarisha watahiriwa kwa majukumu yao mapya ya kiutu uzima.

### 2.3.6 Nyimbo za watoto

Watoto wamejulikana kupenda michezo tangu jadi. Watoto hucheza pasipo kubaguana na kushirikiana kwa kuchukua majukumu tofauti wanapocheza. Baadhi ya nyimbo za watoto zimekiuka utamaduni finyu wa makabila, hasa kutokana na maisha ya mijini, na shuleni. Kwa mfamo, kuna baadhi ya nyimbo za watoto zinazopatikana na kuimbwa bila kubagua. Sifa kuu za nyimbo za watoto ni pamoja na takriri ya silabi, maneno, mishororo na vifungu. Nyimbo hizi pia huandamana na michezo, upigaji wa makofi na maigizo kwa jumla. Nyingi huwa na kiongozi ambaye huanzisha wimbo au igizo nao wenzake wakachukua nafasi mbalimbali. Lengo kuu la nyimbo hizi ni kuwaleta watoto pamoja, kuwachangamsha na pia kuwafunza maadili kupitia ujmbe uliomo. Vilevile, huwasaidia kuyaelewa mazingira wanamoshi.

### 2.3.7 Nyimbo za harusi

Nyimbo hizi zinaweza kuimbwa kabla, wakati au baada ya maarusi kufunga ndoa kwa malengo yafuatayo.

i) Kuwashauri maarusi.

ii) Kuwatayarisha kwa maisha ya ndoa.

iii) Kuwasifu maarusi na wazazi wao.

iv) Kuisifu ndoa kwa ujumla.

Nyimbo hizi pia huimbwa wakati wa kuwasindikiza wachumba kabla ya kufunga ndoa kanisani, na kupokezana kwa zamu. Zipo nyingine ambazo huimbwa kuwasifu wazazi wa maarusi. Kwa jumla, nyimbo za harusi huonyesha furaha na wakati mwingine masikitiko kwa upande wa jamii ya msichana.

### 2.3.8 Nyimbo za mapenzi

M'Ngaruthi (2008) anasema kuwa, mapenzi ni hisia nzito isiyoweza kuelezeka kikamilifu kwa maneno au lugha yoyote. Tamaduni tofauti zina njia tofauti za kuelezea hisia hii ya ajabu. Mara nyingine mapenzi hujaa furaha na buraha isiyopimika ilhali wakati mwingine mapenzi yayo hayo huelezwa kwa machungu hasa na wale waliosalitiwa na mapenzi, hivyo waimbapo huyakashifu na kuonyesha chuki na kisasi kwa waliowatenga na kuwatesa kimapenzi. Lugha iliyotumika na ujumbe hutegemea waimbaji binafsi, umri wao, jinsia, mazingira, na muktadha. Jinsi wachumba wataimbiana ni tofauti na jinsi mke atamwimbia mumewe.

Nyimbo za mapenzi zinapoimbwa, wahusika hudihirisha hisia zao kwa kutabasamu, kucheka au hata kutokwa na machozi, machozi haya yanaweza kuwa ni ya kuonyesha hali ya huzuni labda kama mhusika amempoteza mpenzi wake au dhiki ilyomkumba. Hali kadhalika, machozi pia

yaweza kuwa njia moja ya kuonyesha hali ya furaha isiyo na kifani, hivyo mtu kudondokwa na machozi ya furaha.

### 2.3.9 Nyimbo za kazi (Hodiya)

Kila jamii duniani ina nyimbo za kazi. Mwafrika kwa jumla huithamini kazi na kukejeli uvivu. Wakati kazi tofauti zinafanywa, nyimbo huimbwa ili kupitisha muda, kuifurahia kazi, kuondoa uchovu, kutolea maadili na kwa jumla kurahisisha kazi. Kulingana na M'Ngaruthi (2008), nyimbo za kazi zina baadhi ya sifa kama ifuatavyo:

i) Takriri- maneno na sauti zinazorudiwarudiwa ili kuoana vilivyo na mdundo wa kazi inayoendele-pia pana tanakali za sauti.

ii) Maneno mepesi yaliyo rahisi kujifunza na kuimba palepale.

iii) Maneno, sauti na milio isiyo na maana mradi iweze kujenga mdundo wa nyimbo.

iv) Kupokezana-kiongozi wa wimbo kupokezana wimbo na wenzake.

v) Madoido na vigelegele ili kufanya wimbo kuvutia.

Msamiati, wahusika na maudhui katika nyimbo za kazi hutegemea aina ya wimbo. Kwa mfano, Wamaasai ambao bado wanauthamini ufugaji wanapoimba nyimbo kuhusu mifugo yao, maudhui yao hulenga mifugo malishoni au wanapotoka malishoni. Waswahili, katika jamii yao huwa wana nyimbo kama vile kimai (za wavuvi na mabaharia, wawe (za wakulima) na kongozi (za kusherehekea kufika mwishoni mwa mwaka/kukoga mwaka). Nyimbo hizo zinapoimbwa, wahusika hutolea hisia zao kuhusu maswala husika.

### 2.3.10 Nyimbo za matanga/mbolezi

Nyimbo hizi huimbwa kuomboleza mtu aliyefariki na hutegemea utamaduni wa wanaohusika. Katika tamaduni nyingi hasa za kiafrika, hawakuamini kuwa mtu angekufa tu ikwa wakati wake wa kufa ulikuwa umefika. Hivyo mtu anapofariki, nyimbo hizi huimbwa wakidai kuwa marehemu alirogwa, au ameuawa kwa kuumizwa na mtu au mnyama. Hivyo, walipoimba nyimbo hizi walimlaani yeyote ambaye walidhani kuwa alikuwa ametenda kitendo hicho. Nyimbo hizi pia huimbwa kumsifu marehemu kwa wema wake alipokuwa hai, na vilevile hutumika kuwafariji waliofiwa. Katika kuimba nyimbo za mbolezi, nyimbo za dini pia huimbwa kuwafahamisha watu kuwa kifo ni mapenzi ya Mungu, na kila mmoja atapitia njia hiyo

Nyimbo za matanga pia hutegemea umri na umashuhuri wa marehemu. Watu mashuhuri hutungiwa nyimbo maalum na baadhi ya nyimbo hizo hubaki kumbukumbuni kwa muda mrefu. Kila jamii huwa na nyimbo mashuhuri zinazoimbwa akati wa matanga. Kwa mfano, katika kuashiria huzuni, na kumuaga aliyetangulia.

### 2.3.11 Nyimbo za kishujaa

Nyimbo hizi ziliimbwa nyakati za kupigania uhuru na mataifa mbalimbali ya kiafrika. Katika jamii za kiafrika, wakati mwingine palitokea vita, hivyo kuna watu walioongoza katika kupigana vita hivi, na hatimaye kuibuka washindi. Hivyo, waliteuliwa kuwa mashujaa katika jamii hizo na kutungiwa nyimbo za kuwasifu. Kulingana na M'Ngaruthi (2008) nyimbo za kishujaa ziliimbwa kwa malengo tofauti kama vile;

i) Kuwaombea wanaoenda vitani mafanikio kabla hawajaondoka.

ii) Kujitia moyo-hapa wimbo uliimbwa na mashujaa wenyewe.

iii) Kuwatisha maadui.

iv) Kushangilia ushindi.

v) Kuwakashifu wasaliti na kuwasifu mashujaa.

vi) Kuhifadhi kumbukumbu za yaliyotendeka nyakati za vita.

### 2.3.12 Nyimbo za kizalendo

Mzalendo ni mtu anayependa nchi yake kwa dhati. Nyimbo za kizalendo huonyesha mapenzi makuu aliyonayo mtu kwa nchi. Pia hutumiwa kuwasifu viongozi na kueneza propaganda kuwahusu au kuhusu vitendo vyao. Wimbo wa taifa yetu ni mfano wa nyimbo za kizalendo. Wimbo huu huanza kwa maombi kwa Mungu kisha huendelea kutoa mashauri mbalimbali kwa wananchi ili waishi kwa mshikamano na kulinda nchi yetu. Kashfaa pia hutendwa kupitia nyimbo hizi hasa kwa wale wanaokisiwa kuwa maadui au wasasliti wa serikali. Nyimbo hizi hutungwa kulingana na kiongozi aliye mamlakani na pia hutegemea matukio na utenda kazi wa kiongozi huyo. Nyimbo hizi huwa na athari kwa muda mfupi tu, kutegemea matukio ya kisiasa.

### 2.3.13 Nyimbo za tambiko

Mwafrika katika asili yake aliamini Mungu na miungu, hivyo palipotokea janga au tatizo lolote, palikuwa na haja ya kufanya tambiko. Wakati tambiko ilikuwa ikifanywa, nyimbo mbalimbali za kumsihi Mungu na miungu ziliimbwa. Nyimbo hizi zilidhamiriwa kuonyesha mshikamano wa jamii husika, na pia unyenyekevu kwa Mungu. Jamii mbalimbali kama vile Wamaasai, Wagikuyu wangejitolea kutoa dhabibu kwa Mungu ili awape mvua ya kujikimu pamoja na mifugo yao. Nyimbo hizi zinapatikana katika ngoma za pungwa kwa waswahili, katika miviga kama vile shughuli za kaya kwa Wamijikenda au Njuri Ncheke kwa Wameru.

## 2.14 HITIMISHO

Kwa jumla, kuna aina nyingi za nyimbo na hatuwezi kamwe kutaja au kuzijadili nyimbo za aina zote kwani utamaduni wetu ni mpana sana. Nyimbo huchukua muktadha tofauti kutegemea mambo yafuatayo;

i) Umri wa washiriki au hadhira.

ii) Jinsia-wake au waume.

iii) Shughuli inayohusishwa na nyimbo hizo.

iv) Mandhari- mazingira, hali au wakati.

# SURA YA TATU

# UCHANGANUZI WA MASUALA YA UPOLE KATIKA MATINI TEULE YA NYIMBO ZA MUNISHI: MTAZAMO WA NADHARIA YA UPOLE YA BROWN NA LEVINSON

## 3.0 UTANGULIZI

Katika sura ya pili tulishughulikia suala la nyimbo kwa jumla na tukaangazia nyimbo katika fasihi simulizi kiundani kwani utafiti wetu unahusu fasihi simulizi. Katika sura hii ya tatu, tutashughulikia suala la upole kwenye matini teule ya nyimbo za Munishi. Nyimbo zimerekodiwa katika lugha ya Kiswahili kwenye kanda na kuandikwa.

## 3.1 SUALA LA UPOLE KWENYE NYIMBO ZA DINI KWA JUMLA

Nyimbo za dini zina majukumu makubwa katika jamii yoyote ile. Majukumu haya huathiri mitazamo ya wanajamii kuhusiana na maisha yao na shughuli zao za kimaisha kwa ujumla. Nyimbo hizi zina mawaidha na mafunzo yanayowahusu watu wote katika jamii. Nyimbo za dini huhimiza watu kuishi kwa imani na misingi ya kiungu. Huhimiza jamii yote kuishi pamoja na hushirikisha jamii nzima. Huu ni mkakati wa upole chanya kwa jamii nzima kutokana na kushirikishwa kwao.

Maneno yanayotumiwa katika nyimbo za dini ni ya kimafumbo na yaliyojaa misemo na methali. Huu nao ni mkakati wa upole hasi ambapo lugha hii isiyo ya moja kwa moja hutumiwa kupitisha ujumbe kwa kupunguza makali yake; ni mkakati wa kuwa nje ya rekodi ambao unakusudia kuokoa uso hasi wa jamii. Jamii hushauriwa kipitia nyimbo za dini kuwa na utu, kuwa watu wanaojali majirani wao, kuishi kwa undugu miongoni mwa mengine. Mambo haya hutolewa

kupitia kwa mikakati ya upole hasi; kuwa nje ya rekodi na kuwa kwenye rekodi kama vile tutakavyorejelea baadaye. Vilevile, washiriki husifiwa kwa kuwa na ujasiri kama wa Yesu Kristu katika dini ya kikristu au kuwa na ujasiri kama wa Mohammed katika dini ya kiislamu. Huu ni mkakati wa upole chanya unaolenga kuheshimu uso wao chanya kwa kule kuwasifu.

## 3.2 UPOLE KWENYE MATINI TEULE YA NYIMBO ZA MUNISHI: WIMBO WA MAJI YANA MDUDU

Nyimbo za dini huwatayarisha waumini katika maisha mema ya mbinguni wakati wa siku ya kiyama itakapofika parapanda itakapolia. Maneno yanayopatikana kwenye nyimbo huwapa waumini mashauri ya kuwapa matumaini katika maisha ya sasa na ya baadaye. Ili kufanikisha matumaini haya masuala ya nyuso za wanaohusika huzingatiwa katika utunzi wa nyimbo za dini.

Nyimbo za dini zimegawika katika makundi manne; zile zinazoimbwa kumsifu Mwenyezi Mungu zinazoitwa *Nyimbo za kumsifu Mungu,* nyimbo za maadili, nyimbo za kuabudu na nyimbo za kufariji zinazoimbwa wakati wa majanga katika jamii. Kunayo makundi mengine madogo madogo ya nyimbo za kidini pia.

Nyimbo hizi huwa na majukumu mbalimbali kando na kuwapa waumini matumaini katika maisha. Huisifu jamii ya waumini kwa kuwa jamii ya wenye maono na kuwapongeza waumini kwa kukubali kupeana maisha yao kwa Yesu. Huu ni mkakati wa upole chanya unaolenga kuheshimu uso chanya wa jamii ya waumini. Pia huwakashifu wanaotenda maovu katika jamii, hukejeli waliokataa kuokoka na hushauri jamii ya waumini jinsi ya kuishi maisha mema na kuburudisha. Katika majukumu ya nyimbo za dini, kuna dhana ya kuheshimu na kuokoa nyuso

chanya na kuokoa nyuso hasi zawanaohusika. Pia kuna dhana ya kudhuru nyuso chanya na nyuso hasi za baadhi ya watu katika jamii kama tutakavyoangazia baadaye katika sura hii.

Ili kuelewa vyema kauli hii tutarejelea vipengele vya nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987). Nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) ni nadharia ya kuokoa uso kutokana na matendo ya kutishia uso katika mitagusano ya kijamii. Katika masuala ya kidini, wanajamii hutagusana kupitia kwa nyimbo na matendo. Kwa hivyo kuna uwezekano wa kuwepo na matendo ya kudhuru nyuso za wanaohusika kutokana na mitagusano hii. Hata hivyo katika nyimbo za dini suala hili hushughulikiwa ipasavyo ili nyuso za wanaohusika ziheshimiwe. Ili kuelewa vizuri madai haya tutaangazia vipengele vya upole vya nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1978) ambavyo ni;

### 3.3 UPOLE CHANYA

Huu ni mkakati ambao hujaribu kupunguza tishio la kudhuru uso chanya wa anayezungumziwa au kutendewa jambo fulani. Kutokana na utafiti wetu nyimbo za dini husheheni kipengele cha upole chanya. Kwa mfano katika wimbo wa *Maji yana Mdudu* ulioandikwa hapa chini;

WIMBO WA KWANZA;

*MAJI YANA MDUDU*

Uchimbe kisima wewe mwenyewe
unyewe maji yako peke yako
na usiyashiriki nao wengine ni
utaambukizwa eeh!

Maji ya kisima cha watu wengi
yameingiliwa na mdudu
ukiwa na kiu usiyaonje utaambukuzwa
utaambukizwa eeh!

Na kiu ya maji imeongezeka
watu wanayanywa kila wakati
na yanauzwa kote barabarani nani
utaambukizwa eeh!

Kwa sababu maji yana mdudu
yanapatikana kirahisi
ukipita kote
wacha kuyachota eeh!

Unajua kwa nini?
Kwa sababu pombe na sigara zinaua
wanataka wewe ufe
na wao wanakupatia eeh!

Tena na siku hizi
na hayo maji yaliyoingiwa na mdudu
utapewa bure bila kuomba
ili mfe wote eeh!

Yapo kwenye chupa ndogo na kubwa
watu wanazipenda zile ndogo
wanafikiri zipo salama
wamedanganyika eeh!

Wanazifunika nusunusu
wamefanya hivyo makusudi
ili waamushe kiu ya maji
usidanganyike eeh!

Ndugu jihadhari na maji ya rahisi
kachimbe kisima wewe mwenyewe
ukiwa na kiu uyanywe

maji uliyoyachimba heri.

Dawa ya mdudu hawajaipata

wanaitafuta kotekote

umwamini Yesu

akuokoe amalize kiu

Katika wimbo huu dhana ya upole chanya imedhihirika wazi. Tukichanganua ubeti wa 2 unaoeleza 'maji ya kisima cha watu wengi', huu ni mkakati wa kuheshimu uso chanya wa waumini au jamii kutokana na dhana ya kushirikishwa kwa watu wengi katika jambo muhimu katika jamii. Katika ubeti wa 10, kuna dhana ya kusifu inayojidhihirisha, jina ndugu katika jamii ya kikristu ni jina linalosheneni heshima kwa yule anayeashiriwa. Huu ni mkakati wa upole chanya unaokusudiwa na msanii kuokoa uso chanya wa jamii inayoashiriwa. Hii inatokana na kauli kwamba binadamu yeyote angependa kusifiwa ili uso wake chanya uweze kuheshimiwa. Kila mwanadamu angependa kujihushisha na shujaa katika jamii yake, katika jamii ya kikristu kunaye Yesu ambaye kila mkristu hupenda kujihushisha naye. Katika ubeti wa 11, waumini wanaelezwa na msanii kumwamini Yesu awamalizie kiu. Huu ni mkakati wa upole chanya unaolenga kuokoa uso chanya wa waumini hawa.

Kwa upande mwingine, wimbo huu unadhihirisha pia sifa za kuathiri uso kuwili yaani unaheshimu au unaokoa uso chanya na pia unadhuru uso chanya. Wimbo huu wa *Maji yana Mdudu* una vipengele vya kudhuru uso chanya vilevile. Tukirejelea ubeti wa 9, dhana inayojitokeza ni kuwa wasichana walio na virusi vya ugonjwa hatari wa ukimwi huvalia mavazi

mafupi ili kuamsha uchu wa wanaume wapende kujamiana nao. Hapa nyuso chanya za wasichana wanaorejelewa zinadhurika.mifano mingineyo ni kama yafuatayo;

*Uchimbe kisima wewe mwenyewe*; maana ya mshororo huu ni kwamba, mtu anapaswa kupata mchumba wake binafsi ili asiwe na tabia ya kuchumbia wake au waume wa wengine. Aidha *maji ya kisima cha watu wengi yameingiliwa na mdudu ukiwa na kiu usiyaonje utaambukizwa* mshororo huu unatumika kama tasfida kumaanisha tabia ya kushiriki mapenzi na watu wengi na ukosefu wa uaminifu kwa mchumba wako. Vilevile *kiu ya maji* ni msemo ambao umetumika kama mkakati wa upole kumaanisha hamu ya mapenzi. Fanani anatumia msemo huu kuonyesha jinsi watu wengi walivyo na uchu wa mapenzi hivi kwamba wangeshiriki mapenzi bila kujali maadili ya kijamii na yao ya kibinafsi. *Yapo kwenye chupa ndogo na kubwa watu wanazipenda zile ndogo wanafikiri zipo salama* mshororo huu nao umetumika kwa mkakati wa kuwa nje ya rekodi kwa maana ya baba sukari na mama sukari ambao ni wa umri mkubwa hata ingawa kila jinsia hupendelea wapenzi wenye umri mdogo kuwaliko. Katika muktadha wa nchi ya Kenya kuna wale walioamini kuwa iwapo tayari walikuwa na ugonjwa huo unaozungumziwa katika wimbo, kama wangeshiriki mapenzi wa wasichana wadogo kiumri hasa waliobikira wangepata afueni. *Wanazifunika nusunusu wamefanya hivyo makusudi ili waamushe kiu ya maji usidanganyike.* Kinachorejelewa hapa ni upotovu wa kimaadili umewafanya kina dada hasa kuvaa mavazi yanayowaacha nusu uchi ili waamshe hisia za mapenzi kwa wanaume. *Dawa ya mdudu hawajaipata wanaitafuta kotekote umwamini Yesu akuokoe amalize kiu.* Mshororo huu ni himizo kwa watu wote kuwa wamuamini Yesu ili awaokoe ili amalize kiu hasa kiu ya kufanya mapenzi kiholela pasipo kujali umri au hadhi ya wengine.

## 3.4 UPOLE HASI

Huu ni mkakati ambao hujaribu kupunguza tishio la kudhuru uso hasi wa anayezungumziwa au kutendewa jambo fulani. Katika mkakati wa upole hasi matumizi ya kutumia misemo na methali hujidhihirisha sana. Wakati mwingi lugha itumiwayo hapa sio ya moja kwa moja. Hivyo utapata wasanii wa nyimbo za dini wakitumia mkakati wa kuwa nje ya rekodi ili kuokoa nyuso za wanaohusika.

Katika utafiti wetu nyimbo za dini husheheni kipengele cha upole hasi. Kwa mfano katika wimbo *Maji yana Mdudu*, msanii anawaomba waumini maombi mbalimbali. Katika msitari wa kwanza msanii anawaomba waumini wachimbe visima wao wenyewe wanywe maji yao peke yao. Mbinu ya usafidi/ tasfida imetumiwa katika ombi hili ambao ni mkakati wa upole hasi ambao unalenga kuokoa uso hasi wa waumini. Waumini wanaambiwa waoe wake wenyewe na wafanye ngono na wake zao wenyewe kwani wakishiriki na wengine ni hatari. Katika jamii ya kidini neno kufanya ngono lina makali na linaweza kudhuru uso hasi wa anayeambiwa au wa jamii kwa ujumla hivyo msanii akatumia kunywa maji ili kupunguza makali hayo na basi kuokoa uso hasi wa jamii. Katika ubeti wa nne na pia anwani ya wimbo ni *Maji yana Mdudu* ni mbinu ya tasfida ambapo ingawa angetumia maneno aliyoashiria angeingilia uso hasi wa wanawake kwani alimaanisha kuwa wanawake wamepata virusi vya ukimwi na wako tayari kufanya ngono na wanaume bila malipo ili wawaambukize. Hivyo mbinu ya tasfida iliyotumiwa na msanii Munishi katika wimbo Maji yana Mdudu ulikuwa mkakati wa upole hasi uliokusudiwa kuokoa uso hasi wa waumini na jamii kwa ujumla.

### 3.5 KUWA NJE YA REKODI

Huu ni mkakati wa upole hasi unaodhamiria kuokoa uso hasi. Katika wimbo wa *Maji yana Mdudu,* Munishi anawapa waumini mawaidha kwa mtindo wa wimbo. Mtu kupewa mawaidha kama haya ni kitendo kinachotishia kudhuru uso hasi wa waumini na jamii itakayosikiliza wimbo huu kwa ujumla. Binadamu angependa asiingiliwe au kuombwa hivyo kitendo cha kuwapa waumini mawaidha ni kitendo cha kutishia uso hasi wa waumini hawa. Hata hivyo Munishi anatumia misemo ili kupunguza makali ya kudhuru uso hasi wa jamii. Matumizi ya misemo na lugha isiyo ya moja kwa moja ni mkakati wa kuwa nje ya rekodi unaodhamiria waumini wanaambiwa wasichana wanene na wembamba, wembamba hukimbiliwa na wanaume ili hali wao ndio waliobeba ukimwi. Wimbo wote wa *Maji yana Mdudu* ni wimbo wa kimafumbo katika matumizi yake ya maneno msanii huyu aliteua maneno ya kimafumbo kama mkakati wa upole hasi unaolenga kuokoa uso hasi wa waumini.

### 3.6 KUWA KWENYE REKODI

Huu ni mkakati wa upole hasi. Mkakati huu kwa kawaida hutumiwa na wazungumzaji walio na uelewa wa karibu na hadhira yao. Kutokana na mkakati huu kuna uwezekano wa kusema jambo moja kwa moja kwa hadhira. Hali hii huenda ikadhuru uso hasi wa hadhira iwapo watu hawa hawana uelewa wa karibu. Katika wimbo wa *Maji yana Mdudu*, msanii ametumia mkakati wa kuwa kwenye rekodi hasa pale anaposema "utapewa bure mfe wote" huu ni ujumbe ambao ni mzito na unaoweza kudhuru uso hasi wa wanaoambiwa. Kutokana na kauli kwamba hadhira ya msanii ni wakristo ambao wana uhusiano na uelewano wa karibu naye, ujumbe huu haungedhuru nyuso hasi zao.

## 3.7 HITIMISHO

Katika sura hii tumeshughulikia suala la upole kwenye matini teule ya nyimbo za Munishi; wimbo wa *Maji yana Mdudu* tukirejelea upole chanya na upole hasi. Tumechanganua mikakati ya kuheshimu nyuso za wanaohusika na pia mikakati ya kuokoa nyuso za wanaohusika katika wimbo wa *Maji yana Mdudu*. Tumechanganua mikakati hii ili kubainisha suala la upole katika wimbo ulioimbwa na Munishi wa *Maji yana Mdudu*. Katika uchanganuzi wetu tulirejelea nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987).

# SURA YA NNE

# 4.0 UPOLE KWENYE MATINI TEULE YA NYIMBO ZA MUNISHI: WIMBO WA MALEBO

## 4.1UTANGULIZI

Katika sura ya tatu tulishughulikia suala la upole kwenye matini teule ya nyimbo za Munishi: wimbo wa Maji yana Mdudu. Katika sura hii ya nne, tutashughulikia suala la upole kwenye matini teule ya nyimbo za Munishi: wimbo wa Malebo. Wimbo umerekodiwa katika lugha ya Kiswahili kwenye kanda na kuandikwa.

WIMBO WA PILI;

*MALEBO*

Nina huzuni rohoni, mimi siimbi nalia,
Namlilia Malebo amekataa kuokoka,
Nilizoimba ni nyingi nikimuonya Malebo,
Bado hajabadilika, sasa siimbi ninalia.

Enyi wangu rafiki tuliyesoma pamoja,
Michezo ya utotoni tuliicheza pamoja,
Sasa ni watu wazima na mimi nimeokoka,
Malebo nikimwambia ye anaruka akimanga.

Si yeye peke ninao wengi rafiki,

Nilimwambia nilimwambia kimbele kwenye kaseti ya pili,

Wengine wamekubali wamemwamini mwokozi,

Yesu amewasamehe amebakia Malebo.

Tangu zamani huwa akinitafuta,

Aninunulie chang'aa, bangi, sigara na bia,

Nikimwambia Malebo ninunulie chakula,

Matusi kanitukana, amelalia masikio.

Amenitusi Malebo, uongo kaninenea

Mimi nimemsamehe, najua tatizo lake,

Yeye mtumwa wa dhambi, anataka ukombozi,

Akataka kukubali Yesu atamwokoa.

Nakuita Malebo uje kwa Yesu utubu,

Yeye ni mwenye huruma atakusamehe kabisa,

Jina lako la Malebo litaandikwa mbinguni,

Takuwa kiumbe kipya, ya kale yote tapita.

Mkumbuke Mrefu alivyokuwa mbaya,

Tangu alipokubali kumpa Yesu maisha,

Ameshambadilisha sio Mrefu wa kale,

Sasa anaihubiri injili yake Mwokozi.

Nawajua vizuri Pili na Tatu pamoja,
Walivyokuwa wakali watoto wa mtaani,
Sasa wameshaokoka wamechanua vizuri,
Wote wameshaolewa wana watoto nyumbani.

Wameshanawa mikono damu yako si daima,
Yesu anayekupenda njoo kwake anakuita,
Unanijua vizuri sina haja kueleza,
Yesu amenibadilisha nawe atakubadilisha.

Anakuita ulivyo uje akubadilishe,
Wacha kutia mashaka anajua kazi yake,
Kazi yako kuamini kutubu makosa yako,
Na Yesu atakusamehe na kukuosha kabisa.

Hima njoo kwa haraka wacha kusita Malebo,
Ona ulivyochakaa, meno sita wametoa,
Wale uliowadanganya ukawaibia mapesa,
Wengine wameshaapa watakung'oa mengine.

Sio wote wapole kama unavyoniona,

Pesa ulizonirusha mimi nimenyamaza kimya,

Sasa wale wazaire uliowaibia madola,

Wamesema wakikuona macho yako watang'oa.

Najua maskani unapoishi Malebo,

Jijini Dar-es-salama pepo ya makurumbasi,

Pale mjini Arusha uko ungali nicheki,

Na jina la Nairobi watakupata Majengo.

Pote nimezunguka sijakuona kabisa,

Wazazi wananisumbua hawakuoni nyumbani,

Mkeo yule wa tano anakutaka nyumbani,

Wale uliowafukuza wote pia wamerudi.

Nakuita Malebo uje kwa Yesu utubu,

Yeye ni mwenye huruma atakusamehe kabisa,

Jina lako la Malebo litaandikwa mbinguni,

Takuwa kiumbe kipya, ya kale yote tapita.

**4.2 UPOLE CHANYA**

Huu ni mkakati ambao hujaribu kupunguza tishio la kudhuru uso chanya wa anayezungumziwa au kutendewa jambo fulani. Kutokana na utafiti wetu nyimbo za dini husheheni kipengele cha upole chanya. Kwa mfano katika wimbo huu wa Malebo ulioandikwa hapa juu.

Katika wimbo huu dhana ya upole chanya imedhihirika wazi. Tukichanganua ubeti wa 2, kuna matumizi ya dhana ya wingi au kushirikishwa. Msanii anaelezea marafiki zake waliosoma na kucheza pamoja michezo ya utotoni mambo ya Malebo. Katika mkakati wa upole chanya kila binadamu angependa kutambulika na kuhusishwa katika shughuli za kijamii, sasa wakati msanii anapotambua marafiki zake na kutaja kuwa walicheza pamoja utotoni ni mkakati wa upole chanya unaolenga kuheshimu uso chanya wa marafiki zake. Binadamu yeyote yule hupenda kuhusishwa na shujaa katika jamii yake ili atambulike. Katika wimbo wa Malebo msanii anamwita Malebo aje kwa shujaa wa wakristu Yesu mwenye huruma aweze kumwokoa katika ubeti wa 6 na 15. Ile hali ya kumwita Malebo kwa Yesu ni mkakati wa upole chanya unaokusudia kuuokoa uso chanya wa Malebo.

## 4.3 UPOLE HASI

Upole hasi ni mkakati wa uso hasi. Uso hasi ni madai ya kimsingi ya kila mwanajamii ambapo kila mwanajamii hataki kuingiliwa, kuombwa au mtu mwingine kujikaribisha kwake. Kila mwanajamii anadai haki ya uhuru wake katika jamii. Uso hasi unaweza kupotezwa iwapo mtu atajiingiza katika mambo ya mtu mwingine bila hiari yake, kumwomba mtu kitu chake na hataki kuombwa au kujikaribisha kwa mtu ambaye hajisikii kukukaribisha.

Upole hasi ni mkakati ambao hujaribu kupunguza tishio la kudhuru uso hasi wa anayezungumziwa au kutendewa jambo fulani. Katika mkakati wa upole hasi matumizi ya kutumia misemo na methali hujidhihirisha sana. Wakati mwingi lugha itumiwayo hapa sio ya moja kwa moja.

Katika utafiti wetu nyimbo za dini husheheni kipengele cha upole hasi. Kwa mfano katika wimbo wa Malebo, msanii anaingilia maisha ya Malebo ambapo Malebo anawakilisha watu katika jamii ambao hawajaokoka na ambao huishi maisha yanayoonekana ni kinyume na matarajio ya waliookoka. Msanii anaingilia maisha yao ya kunywa pombe, bangi na sigara. Pia anawaomba wayaache maisha hayo na wamrudie Yesu. Haya yote ni mambo yanayoweza kudhuru uso hasi wa wale ambao hawajaokoka. Ili kupunguza tishio la kudhuru uso hasi wa hawa watu msanii Munishi amewaita kwa jina la kimajazi Malebo badala ya kuwaita kwa majina yao moja kwa moja. Katika beti zote za wimbo wa Malebo mtunzi hajatumia lugha ya moja kwa moja bali ametumia lugha fiche ili kupunguza athari za ujumbe wake kwa jamii.

## 4.4 KUWA NJE YA REKODI

Mkakati huu hutumia lugha isiyo ya moja kwa moja na humwepushia mzungumzaji uwezekano wa kulazimisha. Mzungumzaji huteua maneno yasiyo ya moja kwa moja na kuyatumia kupitisha ujumbe wake kwa hadhira na hadhira ikaelewa na kumfanyia atakavyo bila kuhisi kuingiliwa uso hasi. Wakati mwingine mtu hufanya matendo fulani ili hadhira ikufanyie unavyotaka. Matendo ya mtu yanaweza kuashiria anachotaka au anachoomba.

Katika utafiti wetu, msanii Munishi anataka Malebo aokoke, awache chang'aa, sigara na bia, arudi nyumbani kwa wazazi wake na awarudie wake zake. Kutokana na matakwa haya ya Msanii, kuna uwezekano wa uso wa Malebo ambaye anawakilisha makafiri katika jamii kutishwa. Hata hivyo msanii ameteua maneno yasiyo ya moja kwa moja kupitishia ujumbe huu kwa jamii hii ili isionekane kulazimishwa. Kwa mfano katika ubeti wa tisa anasema Yesu

anakupenda njoo kwake anakuita, haya ni maneno ya kushawishi mtu kubadili mienendo yake bila kuambiwa moja kwa moja. Pia msanii anasema kuwa Yesu amembadilisha na anaishi maisha mema, huu vile vile ni mkakati wa kuwa nje ya rekodi unaonuia kuuokoa uso hasi wa anayezungumziwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Munishi anataka watu waokoke lakini hawaambii moja kwa moja anatumia mfano wake na mifano ya Pili na tatu waliookoka na kupata watoto ili watu waone haja ya kuokoka bila kuhisi kulazimishwa.

## 4.5 KUWA KWENYE REKODI

Huu ni mkakati wa upole hasi. Mkakati huu kwa kawaida hutumiwa na wazungumzaji walio na uelewa na maingiliano ya karibu na wazungumziwa. Katika mkakati huu kuna kusema jambo moja kwa moja kwa wazungumziwa. Hali hii huenda ikadhuru uso hasi wa wazungumziwa iwapo watu hawa hawana uelewa wa karibu. Katika wimbo wa Malebo, msanii ametumia mkakati wa kuwa kwenye rekodi hasa pale anaposema "Nakuita Malebo uje kwa Yesu utubu" ubeti 15 msitari wa kwanza. Hapa ni wazi kwamba kunayo makosa ambayo Malebo ameyafanya na anaambiwa moja kwa moja atubu. Kwa vile hawa wote; msanii na Malebo ni watu walio na uelewano wa karibu huenda Malebo asipate madhara ya uso wake hasi.

## 4.6 HITIMISHO

Katika sura hii tumeshughulikia suala la upole kwenye matini teule ya nyimbo za Munishi wimbo wa *Malebo* tukirejelea upole chanya na upole hasi. Tumechanganua mikakati ya kuheshimu nyuso za wanaohusika na pia mikakati ya kuokoa nyuso za wanaohusika kwenye wimbo wa *Malebo*. Tumechanganua mikakati hii ili kubainisha suala la upole katika matini teule ya nyimbo za Munishi; wimbo wa *Malebo*. Katika uchanganuzi wetu tulirejelea nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987).

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 UTANGULIZI

Katika utafiti huu madhumuni yalikuwa ni kuchunguza suala la upole kwenye matini teule ya nyimbo za Munishi; wimbo wa *Maji yana Mdudu* na *Malebo*. Lengo letu lilikuwa ni kubainisha kwamba kuna suala la upole katika matini teule ya nyimbo za Munishi; wimbo wa *Maji yana Mdudu* na *Malebo*. Tumechanganua nyimbo mbili za Munishi ambazo ni nyimbo za dini kwa sababu dini ni moja wapo ya taasisi zinazotekeleza majukumu muhimu katika jamii kama vile kusisitiza suala la upole na heshima katika jamii.

## 5.1 HITIMISHO

Tulitaka kuthibitisha ukweli wa nadharia tete kwamba kuna mikakati mbalimbali ya kuokoa uso chanya kwenye matini teule ya nyimbo mbili za Munishi. Pia tulitaka kuthibitisha kwamba kuna mikakati mbalimbali ya kuokoa uso hasi kwenye matini teule ya nyimbo mbili za Munishi. Matini teule ya nyimbo mbili za Munishi hufumbata dhana ya upole na heshima kwa wanaohusika katika jamii ya wakristu. Kwa kuzingatia nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) tumeweza kuangazia suala la upole kwenye matini teule ya nyimbo mbili za Munishi hasa kwa kuzingatia vipengele viwili vikuu vya nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987): upole chanya na upole hasi. Tumeweza kuthibitisha kwamba kuna mikakati mbalimbali ya kuokoa uso chanya kwenye matini teule ya nyimbo mbili za Munishi. Pia tumethibitisha kuwa kuna mikakati mbalimbali ya kuokoa uso hasi kwenye matini teule ya nyimbo mbili za Munishi.

Vile vile, tulitaka kuthibitisha kuwa nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) inatosheleza kuchanganua matini teule ya nyimbo mbili za Munishi. Tumeweza kuthibitisha kwamba nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) inatosheleza kuchanganulia suala la upole kwenye matini teule ya nyimbo mbili za Munishi.

Katika sura ya pili, tulichunguza kwa undani dhana ya nyimbo, aina za nyimbo na majukumu ya nyimbo kwa ujumla. Ni wazi kwamba nyimbo ni sehemu muhimu ya jamii na kila jamii inaenzi nyimbo zinazopatikana katika jamii husika. Nyimbo husawiri jamii kwa nyanja zote huku ikiangazia yanayomkumba mwanajamii yawe mema au maovu. Ni kupitia nyimbo ambapo tunaifahamu jamii husika kihistoria, mila na desturi kwani jamii yoyote ile ni historia yake, mila, desturi na tamaduni zake. Kwa hivyo nyimbo humulika mema ili yaweze kusifiwa na kuigwa na kizazi kipya cha jamii. Vilevile nyimbo huangazia maovu katika jamii ili yaweze kukashifiwa na kurekebishwa yasiweze kuendelea kukita mizizi katika jamii.

Katika sura ya tatu, tumeshughulikia kuchambua matini teule ya nyimbo za Munishi; wimbo wa *Maji yana Mdudu.* Kwa kuzingatia nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987), tumebainisha kwamba kuna suala la upole kwenye wimbo wa *Maji yana Mdudu.* Tumeshughulikia wimbo huu kiundani na kuthibitisha kwamba kuna dhana ya upole. Mkakati wa upole chanya umepewa kipaumbele na msanii Munishi kwenye wimbo wa *Maji yana Mdudu.* Vilevile upole hasi ulizingatiwa na Munishi katika wimbo huu hasa kupitia kwa mikakati ya kuwa nje ya rekodi na kuwa kwenye rekodi ili kuokoa uso hasi wa wanaohusika.

Katika sura ya nne, tumeshughulikia kuchambua matini teule ya nyimbo za Munishi; wimbo wa *Malebo*. Kwa kuzingatia nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987), tumebainisha kwamba kuna suala la upole kwenye wimbo wa *Malebo*. Tumeshughulikia wimbo huu kiundani na kuthibitisha kwamba kuna dhana ya upole. Mkakati wa upole chanya ulipewa kipaumbele na msanii Munishi kwenye wimbo wa *Malebo*. Vilevile upole hasi ulizingatiwa na Munishi katika wimbo huu hasa kupitia kwa mikakati ya kuwa nje ya rekodi na kuwa kwenye rekodi ili kuokoa uso hasi wa wanaohusika.

Katika uchanganuzi wetu tumebainisha kwamba, tukizingatia nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987), katika utunzi wa matini teule ya nyimbo mbili za Munishi kuna suala la uso ambalo huzingatiwa ili kuheshimu nyuso za wanaohusika. Bila suala la upole kwenye nyimbo za Munishi, nyuso za watu katika jamii hasa wakristu zingekuwa zimedhurika na mwishowe nyimbo hizi zingalipoteza umaarufu wake katika jamii ya kikristo. Tumeng'amua kwamba idadi kubwa ya maneno yanayotumiwa kwenye nyimbo za Munishi ni yenye maana fiche.

## 5.2 CHANGAMOTO TULIZOKUMBANA NAZO KATIKA UTAFITI WETU

Utafiti wetu ulifanywa nyanjani. Sampuli yetu ilikuwa sampuli lengwa (purposive sampling). Tulizuru makanisa mbalimbali katika mjini ya Nakuru kama kanisa la P.A.G. Hii ni kwa sababu nyimbo za Munishi ni nyimbo za dini hivyo tungepata habari toshelevu kutoka kwa makanisa. Baadhi ya waumini tuliowahoji walikuwa na muda mchache wa kutuhudumia na tukapata shida kupata habari zote tulizotarajia.

Baadhi ya wachungaji wa makanisa walitukashifu na kutulaani kuwa ni dhambi kufanya utafiti katika mambo ya Mungu. Walilalamika kwamba mambo ya Mungu sio ya mchezo wa wasomi na hayastahili kutiliwa shaka au kuulizwa ni kwa nini.

Siku ya kwanza tulijaribu kuwahoji wasimamizi wa kanisa la *Full Gospel* mjini Nakuru na wakatueleza kwamba walikuwa na jukumu la kuwashughulikia waliotaka uponyaji wa kiroho na iwapo tulitaka kufanyiwa mengine basi tuje siku nyingine. Tulivyorudi huko siku iliyofuata hadithi ilikuwa ileile.

Baadhi ya wachungaji tuliowauliza walitaka kujua iwapo tumeokoka kwanza ndipo watuhudumie na iwapo hatukuokoka walituwekea masharti kwamba tumpokee Yesu kwanza. Ilibidi tujifanye tumekubali kuokoka ili tupate habari kuhusu nyimbo za Munishi.

Muda tulikuwa nao wa kufanya utafiti ulikuwa mchache kuweza kupata habari tuliyotaka kwani kwa waumini wengi, kando na kupatikana katika makanisa walitueleza kwamba walitakiwa kuzishughulikia familia zao kwa kuzitafutia riziki.

Kwa hivyo mambo haya yalitatiza utafiti wetu. Hata hivyo yale maelezo waliyotupatia yaliweza kutusaidia katika utafiti wetu.

## 5.3 MAPENDEKEZO

Tulichukua mwelekeo huu wa kutathmini suala la upole kwenye matini teule ya nyimbo za Munishi kwa nia ya kubainisha kwamba suala la upole huzingatiwa kwenye nyimbo hizi. Kulingana na mawazo ya wengi kwamba nyimbo za dini hazizingatii suala la upole bali hutumia vitisho ili kuwalazimisha watu kumpokea Yesu, jamii inastahili kuelewa kwamba nyimbo za dini zina majukumu mengi katika jamii na zinastahili kupewa mchango chanya kwa kuzitathmini kiundani. Ni vyema kufanya utafiti zaidi wa tanzu za fasihi simulizi ambazo hazijafanyiwa utafiti wa kina kama vile masimulizi, maigizo, semi, ngomezi, ushairi na mazungumzo.

Tulichagua kipengele cha upole kwenye matini teule ya nyimbo za Munishi. Ilivyobainika ni kwamba suala la upole huzingatiwa kwenye nyimbo hizi. Lugha inayotumiwa katika nyimbo huwa teule na hai inayotekeleza majukumu mengi katika jamii ya kikristu. Kutokana na lugha hii, jamii ya kikristu imefanikiwa katika mitagusano yao mbalimbali ya kimaisha na kufanya jamii kuishi kwa umoja na upendo. Kwa hivyo tungependekeza vipengele vingine vya nyimbo pia vifanyiwe utafiti kwa mfano fani, maudhui na mitindo.

Tulichukua mwelekeo wa suala la upole kwenye matini teule ya nyimbo za Munishi. Hata hivyo pana mielekeo mbalimbali inayoweza kuchukuliwa kuangazia tanzu zingine za fasihi simulizi katika dini kama vile ushairi, ulumbi na maigizo kama zinavyojitokeza katika dini.

## MAREJELEO


Austin, J (1962) . *How to do Things with Words*. London: Oxford University Press

Bukenya, A and Nandwa, J (1983). *African Oral Literatre for School*, Nairobi: Longman, Kenya

Dorch, S (1965), *Classical Literacy Criticism*: Harmonsworth: Penguine Books Limited

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. London: Oxford University.

Finnegan, R. (1992) *Oral Traditions and Verbal Arts Guide to Research*. London: Routledge

King'ei, K. (1993). *Langauge , Culture and Communication. The Role of Swahili Taarab Songs in Kenya* 1963- 1990 U.M.L Dissertation Information of Bells Howen Informaiton Company of Michigan, USA

King'ei, K. et al (2005) *Msingi wa Fasihi Simulizi.* Nairobi; Kenya Literature Bureau.

Kirumbi, P.S (1975) *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi Shungwaya Publishers

Leech, G (1983) *Principles of Pragmatics*. Singapore: Longman Publishers.

Levinson, S.C (1983) *Pragmatics*: Cambridge: Cambridge University Press.

Marmaridou, S. A (2000), *Pragmatic*, Meaning and Cognition, Amsterdam; John Benjamins Publishing Company

Matteru (1981): *Fasihi Simulizi na Uandisi' Makala ya Semina ya Waandishi wa Kiswahili* Dar-es-Salaam, TUKI

_________ (1979). *' Utafiti, mbinu na ukusanyaji wa Fasihi Simulizi na hatima yake.' Lugha yetu na 34-36 BAKITA* Dar- es-salaam.

Mbiti, J (1991) *Introduction to African Religion*, Nairobi East African Educational Publishers.

Mkonge, M (2008) ' *Literacy Study of Songs of Joseph Kamaru*. Theme and Styles. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

Mulokozi, M (1981) *Nafasi ya Majimbo za Fasihi Simulizi' katika Jamhuri inayobadilika' Makala ya Semina ya Fasihi Simulizi.* Dar- es- Salaam: TUKI;

_________(1983) *' Utafiti wa Fasihi Simulizi katika Makala ya Semina ya Kitaifa ya Waandishi wa Kiswahili III.* Fasihi, Dar- es-Salaam, TUKI.

_________ (1989) *' Fasihi Simulizi,' Mulika Namba 21.* Dar- es- Salaam; TUKI

Ndungo et al (1993) *Nadharia ya Fasihi Simulizi*, Nairobi: University of Nairobi Fress.

New Internaitonal Webster Comprehensive Dictionary of the English Langauge (2001), CBS Publishers and Distributors, New Delhi.

Ngugi (1986), *Decolonizing the Mind, The Policies of African Literaturr*, Nairobi; East African Literature Bureau.

Njogu, K. et al (1999*) Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Nkwera, F (1978) *Sarufi na Fasihi, Sekondari na Vyuo*. Dar- es- Salaam: T.P.H

Penelope, B na Levison, S (1987) *Pragmatics*: London; Cambridge University Press.

Rapando, Y.P (1991). *Maudhui Katika Nyimbo za John Mwale.* Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Thonya, L.M (1978) *Misingi ya Kiswahili*, Dar- es- Salaam. Black Star Agencies

Timammy, R(2002), *Swahili Women's Wedding Songs*: A Stylistic Analysis. Tasnifu ya Ph.D Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Tuki (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*: TUKI, Dar- es- Salaam

Wallek, R. et al (19949) *Theory of Literature*. Harmondsworth Penguin Books

Wamitila, K (2002). *Uhakiki was Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi; Phoenix Publsihers.

Wamitila, K (2003 a). *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books

Wamitila, K (2003b) *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*: Nairobi; Focus Books.

Wardhaugh, R. (1986), *Introduction to Sociolinguistics*, (2nd ed); Cambridge. Blackwell

Wardhaugh, R. (2002*) Sociolinguistic*. (4thd ed) New York: Blackwell.

Yule, G. (1996) *Pragmatics.* London: Oxford University Press

# VIAMBATISHO

WIMBO WA KWANZA;

*MAJI YANA MDUDU*

Uchimbe kisima wewe mwenyewe
unyewe maji yako peke yako
na usiyashiriki nao wengine ni
hatarikubwa eeh!

Maji ya kisima cha watu wengi
yameingiliwa na mdudu
ukiwa na kiu usiyaonje utaambukuzwa
eeh!

Na kiu ya maji imeongezeka
watu wanayanywa kila wakati
na yanauzwa kote barabarani nani
atapona eeh!

Kwa sababu maji yana mdudu
yanapatikana kirahisi
ukipita kote wacha kuyachota eeh.

Unajua kwa nini?
Kwa sababu pombe na sigara zinaua
wanataka wewe ufe
na wao wanakupatia eeh.

Tena na siku hizi
na hayo maji yaliyoingiwa na mdudu
utapewa bure bila kuomba ili mfe wote
eeh.

Yapo kwenye chupa ndogo na kubwa
watu wanazipenda zile ndogo
wanafikiri zipo salama
wamedanganyika eeh.

Wanazifunika nusunusu
wamefanya hivyo makusudi
ili waamushe kiu ya maji usidanganyike
eeh.

Ndugu jihadhari na maji ya rahisi
kachimbe kisima wewe mwenyewe
ukiwa na kiu uyanywe
maji uliyoyachimba heri.

Dawa ya mdudu hawajaipata
wanaitafuta kotekote
umwamini Yesu
akuokoe amalize kiu

WIMBO WA PILI;

*MALEBO*

Nina huzuni rohoni, mimi siimbi nalia,
Namlilia Malebo amekataa kuokoka,
Nilizoimba ni nyingi nikimuonya Malebo,
Bado hajabadilika, sasa siimbi ninalia.

Enyi wangu rafiki tuliyesoma pamoja,
Michezo ya utotoni tuliicheza pamoja,
Sasa ni watu wazima na mimi nimeokoka,
Malebo nikimwambia ye anaruka akimanga.

Si yeye peke ninao wengi rafiki,
Nilimwambia nilimwambia kimbele kwenye kaseti ya pili,
Wengine wamekubali wamemwamini mwokozi,
Yesu amewasamehe amebakia Malebo.

Tangu zamani huwa akinitafuta,
Aninunulie chang'aa, bangi, sigara na bia,
Nikimwambia Malebo ninunulie chakula,
Matusi kanitukana, amelalia masikio.

Amenitusi Malebo, uongo kaninenea
Mimi nimemsamehe, najua tatizo lake,
Yeye mtumwa wa dhambi, anataka ukombozi,
Akataka kukubali Yesu atamwokoa.

Nakuita Malebo uje kwa Yesu utubu,
Yeye ni mwenye huruma atakusamehe kabisa,
Jina lako la Malebo litaandikwa mbinguni,

Takuwa kiumbe kipya, ya kale yote tapita.

Mkumbuke Mrefu alivyokuwa mbaya,
Tangu alipokubali kumpa Yesu maisha,
Ameshambadilisha sio Mrefu wa kale,
Sasa anaihubiri injili yake Mwokozi.

Nawajua vizuri Pili na Tatu pamoja,
Walivyokuwa wakali watoto wa mtaani,
Sasa wameshaokoka wamechanua vizuri,
Wote wameshaolewa wana watoto nyumbani.

Wameshanawa mikono damu yako si daima,
Yesu anayekupenda njoo kwake anakuita,
Unanijua vizuri sina haja kueleza,
Yesu amenibadilisha nawe atakubadilisha.

Anakuita ulivyo uje akubadilishe,
Wacha kutia mashaka anajua kazi yake,
Kazi yako kuamini kutubu makosa yako,
Na Yesu atakusamehe na kukuosha kabisa.

Hima njoo kwa haraka wacha kusita Malebo,
Ona ulivyochakaa, meno sita wametoa,
Wale uliowadanganya ukawaibia mapesa,
Wengine wameshaapa watakung'oa mengine.

Sio wote wapole kama unavyoniona,
Pesa ulizonirusha mimi nimenyamaza kimya,
Sasa wale wazaire uliowaibia madola,
Wamesema wakikuona macho yako watang'oa.

Najua maskani unapoishi Malebo,
Jijini Dar-es-salama pepo ya makurumbasi,
Pale mjini Arusha uko ungali nicheki,
Na jina la Nairobi watakupata Majengo.

Pote nimezunguka sijakuona kabisa,
Wazazi wananisumbua hawakuoni nyumbani,
Mkeo yule wa tano anakutaka nyumbani,
Wale uliowafukuza wote pia wamerudi.

Nakuita Malebo uje kwa Yesu utubu,
Yeye ni mwenye huruma atakusamehe kabisa,
Jina lako la Malebo litaandikwa mbinguni,
Takuwa kiumbe kipya, ya kale yote tapita.